# Nipashe

Jumatatu Septemba 5, 2022 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581059

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

The Guardian digital nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710 LIKE & FOLLOW US







**Mchujo** makada 180 CCM waanza, ACT yapitisha 2

UKURASA 5


INVITATION OF OFFER TO BUY MOLASSES

We have 2000 tons of fresh **Molasses for sale**, produced from our state-of-the-art sugar factory. Interested parties may contact us as per following details with quantity required and offer price.

0786066854 / 0678244770

BAGAMOYO SUGAR


# Binti achinjwa

• **Mwili** watupwa barabarani, chupa ya pombe yakutwa eneo la tukio... *Uk. 2*

## YALIYOMO

UKURASA WA 4

### KANALI AMSHAURI IGP KUUNDA KIKOSI MAALUM CHA MPAKANI

MKUU wa Wilaya ya Rombo mkoani Kilimanjaro amemshauri Mkuu wa Jeshi la Polisi, IGP Camilius Wambura, kuunda kikosi kazi maalum kitakachokuwa na jukumu pekee la kupambana na wahalifu wanaovuka mipaka ya Holili na Tarakea baada ya kufanya uhalifu...

UKURASA WA 4

### MAJERUHI 10 AJALI ILIYOUA WAHAMISHIWA BUGANDO

MAJERUHI 10 wa ajali ya basi lililogongana na lori aina ya Fuso mkoani Shinyanga, wamehamishiwa Hospitali ya Rufani ya Kanda ya Ziwa (Bugando) jijini Mwanza kwa ajili ya kupatiwa matibabu zaidi...




Rais Samia Suluhu Hassan (kulia), akimsikiliza Mkaguzi Mkuu wa Ndani wa Benki ya NMB, Benedicto Baragomwa (kushoto), alipotembelea banda la NMB wakati wa kufunga Tamasha la Kizimkazi visiwani Zanzibar juzi. Rais aliambatana na Mke wa Rais wa Zanzibar, Mariam Mwinyi (wa pili kulia), Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa na Mkuu wa Mkoa wa Kusini Unguja, Rashid Khalid Rashid. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Mwili askofu aliyeanguka kanisani kuagwa leo

UKURASA 2



## Kinana ataka serikali iwajibishwe kiutendaji

UKURASA 2

**MICHEZO** TPLB YAPONGEZA KLABU USAJILI LIGI KUU UK.23

**KABWELA** UK.18

# Kinana ataka serikali iwajibishwe kiutendaji

**Na Waandishi Wetu,** GEITA

MAKAMU Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Bara, Kanali mstaafu Abdulrahman Kinana, amewataka wabunge kuwa wakali kwa kuiwajibisha serikali ili itekeleze miradi ya maendeleo kwa wananchi.

Kadhalika, ameagiza kuwapo na mipango ya ujenzi katika miji kutokana na mingi kutotekelezeka na miji kuendelea kuwa katika hali mbaya.

Aliyasema hayo jana wakati wa kikao cha ndani cha wanachama CCM Mkoa wa Geita, akiwa katika ziara yake ya ukaguzi wa uhai wa chama hicho, utekelezaji wa ilani na kusikiliza kero za wananchi.

Alisema yeye ni miongoni mwa watu anayependa wabunge wawe wakali kwa serikali kuhusu mambo yanayohusu utelekezaji wa kero za wananchi.

Akiwa ameambatana na Katibu wa Itikadi na Uenezi CCM, Shaka Hamdu Shaka, Kinana alikumbusha kuwa chama ndicho kinachokwenda katika uchaguzi na kutaka matatizo ya wananchi yatatuliwe badala ya kutoa majibu rahisi kwa mambo magumu.

"Hiki chama ndicho kitaomba kura, hiki chama ndicho kitapewa viongozi ama kunyimwa na sio serikali. Wale watendaji na watumishi wa serikali wao wapo, ukiwapo wapo, ukiondoka wapo, iwapo mambo hayatakwenda watakaoadhibiwa ni Chama Cha Mapinduzi," alisisitiza.

Alisema Rais Samia Suluhu Hassan anajitahidi na kazi ya urais sio ya mtu mmoja, wabunge wanapaswa kumsaidia ili mambo yaende vizuri na wananchi wanufaike.

Kadhalika alisema, ahadi zilizotolewa zinaposhindwa kutekelezwa, wapinzani wanachukua udhaifu huo na kueleza wananchi CCM ahadi zao ni hewa.

Kuhusu suala la ujenzi wa barabara kwa Mkoa wa Geita, alisema amejifunza mambo mengi katika ziara yake kutokana na kusuasua huku fedha zikiwa zimetengwa kwa ajili ya miradi hiyo.

"Nilikuwa huko Rukwa, Katavi na sasa nipo hapa Geita habari ndio hiyo hiyo hata kama huna uwezo wa kutoa fedha zote basi toeni kiasi halafu tujue umeshindwa na uwaeleze fedha hizo tulikuwa tutoe, lakini zimekwenda mahali pengine hili sio jambo zuri sana," alionya Kinana.

Akizungumzia mipango miji, alishauri kutengwe fedha kwa ajili ya kupanga mji wa Geita ili ufanane na dhahabu iliyopo na kuwakumbusha viongozi kujitahidi kulisimamia suala hilo.

Akipokea taarifa ya malalamiko ya mgogoro wa ardhi mkoani Geita, alisema suala hilo limekuwa tatizo kila anapopita.

Alisema ni muhimu kutafuta njia ya kupata ufumbuzi wa kero hiyo na kwamba atakwenda kuzungumza na Kamati ya Bunge ya Ardhi ili iweze kusaidia.

Akiwa Geita, Kinana alikumbusha na kukemea vitendo vya rushwa, udini na ukabila katika uchaguzi unaoendelea ngazi ya wilaya na mikoa.

Alikuwa akifungua kikao cha viongozi wa mashina (mabalozi) tawi, kata, wilaya na mkoa, mjini Geita.

Alishauri wagombea wote walioomba kugombea nafasi mbalimbali ndani ya chama hicho wapimwe kwa kuzingatia uwezo wao na mchango walioutoa kwa chama bila kutanguliza ukabila, udini na rushwa.

Aliwasisitiza viongozi hao kuzingatia maadili na katiba ya chama hicho.

Alisema wapo wanaCCM wengi wanaogopa kuomba kugombea nafasi mbalimbali ndani ya chama hicho wakihofia kushindwa kutokana na kutokuwa na fedha.

Kadhalika, alisema Mkoa wa Geita bado mpya unahitaji ushirikiano kati ya watendaji wa serikali pamoja na viongozi wa chama ili kufanikisha maendeleo yake.

Aidha, alisema kazi ya Rais Samia Suluhu Hassan ni kutafuta fedha na watendaji wa serikali na madiwani ni kubuni miradi na kusimamia fedha ya miradi ya maendeleo kikamilifu.

Kwa upande wake, Katibu wa Itikadi na Uenezi wa CCM mkoani Geita, David Azaria alisema kauli ya Kinana imekuja kipindi kizuri kutokana na kukithiri kwa matabaka katika chaguzi za matawi na kata zilizofanyika mwaka huu.

■**Imeandikwa na Beatrice Shayo na Alphonce Kabilondo, GEITA**

# Binti auawa kwa kuchinjwa

**Na Vitus Audax,** MWANZA

BINTI ambaye jina lake halijafahamika, amekutwa ameuawa kwa kuchinjwa kwa kitu chenye ncha kali nyuma ya shingo huku mwili wake ukitelekezwa kando ya barabara katikati ya mitaa ya Nyanza, Kata ya Mkolani na Igubinya, Kata ya Nyegezi mkoani Mwanza.

Mwili wa kijana huyo anayekadiriwa kuwa na umri wa kati ya miaka 25 na 35 uliokotwa huko huku pembeni yake kukiwa na chupa yenye pombe.

Tukio hilo lilitokea usiku wa kuamkia jana na kuthibitishwa na wenyeviti wa mitaa hiyo miwili huku chanzo cha mauaji hayo kikiwa bado hakijajulikana na upelelezi wa kubaini wahusika unaendelea kufanywa na Jeshi la Polisi.

Mwenyekiti wa Mtaa wa Igubinya, Ndonho Nzella, aliambia Nipashe kuwa alipokea taarifa hiyo kutoka kwa mashuhuda na kufika eneo la tukio na kuukuta mwili huo ambao haukutambulika.

"Nilipofika eneo la tukio, niliamua kuwajulisha polisi ambao walifika na kuuchukua mwili kwa ajili ya kuuhifadhi hospitalini, utambuzi na uchunguzi ili kujua chanzo na wahusika wa mauaji hayo," alisema Ndonho.

Awali akizungumza na Nipashe jana, Mwenyekiti wa Mtaa wa Nyanza, Barnaba Luswetula, alisema alipokea taarifa za tukio hilo kutoka kwa Ofisa Mtendaji wa Kata yake na kuelekea eneo la tukio.

Barnaba alisema kuwa baada ya kufika eneo la tukio, alikuta tayari mwili wa marehemu umechukuliwa na Jeshi la Polisi kwa ajili ya uchunguzi huku akieleza kuwa tukio hilo ni la pili kutokea katika mtaa huo mwaka huu.

"Hili limekuwa ni tukio la pili kutokea katika mtaa huu, miezi michache iliyopita aliuawa kijana mmoja kwa kukatwa na panga na mwili wake ulitambulika," alisema na kubainisha kuwa Jeshi la Polisi lilishawataarifa kuwa linaendelea kufanya uchunguzi kuhusu matukio hayo," alisema.

Akizungumza na Nipashe kwa simu jana, Kaimu Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mwanza, Gidion Msuya, alithibitisha kutokea kwa tukio hilo.

Alisema mwili huo ulichukuliwa katika eneo la tukio na wanaendelea na kuufanyia uchunguzi ili kuwabaini wahusika.

"Kwa sasa tunaendelea na uchunguzi ili kubaini chanzo cha mauaji hayo pamoja na wahusika, binti huyo mpaka sasa hajatambulika, lakini akitambuliwa tutatoa taarifa kwa wakati," alisema.



Naibu Katibu Mkuu wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC), Mhandisi Steven Mlote (kushoto), akizungumza na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, Vita Rashid Kawawa, wakati kamati hiyo ilipofika makao makuu ya EAC jijini Arusha jana, kupata taarifa ya miradi ya miundombinu inayoratibiwa kwa pamoja kati ya jumuiya hiyo na serikali ya Tanzania. **PICHA: EAC**

# Mwili askofu aliyeanguka kanisani kuagwa leo

**Na Steven William**, MUHEZA

MWILI wa aliyekuwa Askofu wa Kanisa la Anglikana Tanzania (ACT) Dayosisi ya Mpwapwa mkoani Dodoma, George Chiteto, unatarajia kuagwa leo Muheza mkoani Tanga.

Askofu Chiteto alifariki dunia ghafla juzi baada ya kuanguka kanisani muda mfupi baada ya kumaliza mahubiri ya mazishi ya aliyekuwa Rais wa Ushirika wa Mama wa Kikristo wa Kanisa la Anglikana Tanzania (UMASKI), Hilda Lugendo.

Baada ya kuanguka, kiongozi huyo alibebwa na wachungaji na maaskofu waliokuwa katika ibada hiyo na kumwingiza katika gari kisha kumpeleka Hospitali Teule ya Wilaya ya Muheza kwa ajili ya matibabu lakini muda mfupi baadaye ilitangazwa kwamba amefariki dunia. Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana na Mchungaji wa Kanisa la Anglikana Kristo Mfalme lililoko Mtaa wa Madaba wilayani Muheza, Paul Luhinga, shughuli ya kuaga mwili wa askofu huyo itaanza mapema leo katika kanisa hilo.

Hivyo, aliwataka waumini kujitokeza kwa wingi kuuaga mwili wa Askofu Chiteto na kwamba baada ya taratibu za kuaga kumalizika, utasafirishwa kwenda Mpwapwa mkoani Dodoma kwa ajili ya maziko.

Alisema shughuli hiyo ya kuuaga mwili wa Askofu Chiteto itaongozwa na Askofu Mkuu wa Kanisa la Anglikana Tanzania, Mahimbo Mndolwa, na viongozi wengine wa dini, vyama na serikali.

Kamishna wa Tume ya Utumishi nchini, Balozi Adadi Rajabu ametoa salama za rambirambi kwa niaba ya Rais Samia Suluhu, akiwapa pole wafiwa kwa msiba hiyo miwili.

Balozi Rajabu ambaye aliwahi kuwa Mbunge wa Muheza, aliwataka wanafamilia hao kuwa watulivu na wavumilivu katika kipindi hiki kigumu cha msiba na kwamba serikali iko nao katika kipindi hiki cha majonzi.

Katibu Mwenezi mstaafu wa CCM Wilaya ya Muheza, Makame Seif na Mwenyekiti wa Halmashauri ya Muheza, Erasto Mhina, kwa nyakati tofauti walitoa pole kwa ndugu na familia kwa msiba huo.

## TANGAZO


WA kishua
WAKISHUA
WA TIGO
TUNAJUANA
Furahia michongo ya kidigitali kila kona ya Tanzania
tigo
tigo pesa
Boomplay
Pakua au boresha App hizi.
Jipatie Laini ya Tigo.
217028402



Baadhi ya wanachama wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) walioomba kuteuliwa na chama hicho, kugombea ubunge wa Bunge la Afrika Mashariki (EALA) wakisubiri kufanyiwa usaili katika ukumbi wa Jakaya Kikwete mkoani Dodoma. Usaili huo unafanywa na Sekretarieti ya Halmashauri Kuu CCM Taifa na umefanyika kwa siku mbili jana na leo. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Kanali amshauri IGP kuunda kikosi maalum cha mpakani

**Na Godfrey Mushi,** ROMBO

MKUU wa Wilaya ya Rombo mkoani Kilimanjaro amemshauri Mkuu wa Jeshi la Polisi, IGP Camillius Wambura, kuunda kikosi kazi maalum kitakachokuwa na jukumu pekee la kupambana na wahalifu wanaovuka mipaka ya Holili na Tarakea baada ya kufanya uhalifu.

Kanali Hamisi Maiga amesema uhalifu unaoitishia usalama katika maeneo hayo ni uvushaji wa mifugo kutoka nchi jirani na kuvamia mashamba ya wakulima huku wakifanya mauaji, kujeruhi na kupora mali.

Akizungumzia hali ya uhalifu na magendo katika mipaka hiyo inayoitenganisha Tanzania na Kenya, Kanali Maiga alisema nchi hiyo jirani tayari imeanzisha kikosi hicho lakini Tanzania haijafanya hivyo.

Kanali Maiga alikuwa akizungumza na IGP Wambura alipokwenda juzi wilayani Rombo kuzindua Kituo cha Polisi Ngoyoni kitakachotoa huduma kwa vijiji vilivyoko mpakani mwa nchi hizo mbili.

"Ombi langu kwako IGP, Wilaya ya Rombo ukitokea Longido kuja hadi Holili, ina umbali wa kilomita 100. Huu ni umbali mrefu sana, ukilinganisha na wenzetu kule Kenya, wana kitu kinaitwa Border Management Team.

"Hawa ni askari kila kukicha asubuhi na jioni kazi zao ni kurun ule mpaka (kuudhibiti). Kwa upande wetu huku hicho kitu hatuna, kwa sababu polisi tulionao ni wachache na pia hawawezi wakafanya hiyo kazi.

"Mimi ninachokuomba mkuu wangu (IGP), kama inawezekana walau unaweza ukatupa section moja plus (kikosi), wakiwa na gari la patrol (ukaguzi) ili waweze kuudhibiti vizuri huu mpaka, na kwa kufanya hivyo itaisaidia serikali kupata mapato mengi kwenye vituo vyake vya forodha ambavyo ni Holili na Tarakea," aliwasilisha.

Kwa mujibu wa Kanali Maiga, Holili imekuwa kinara wa mapato. Mapato yake yamekuwa makubwa, hayajawahi kutokea ndani ya miaka 10 iliyopita. Tarakea navyo ni hivyo hivyo, licha ya kuwapo tishio hilo la kiusalama na uhaba wa askari polisi.

"Kama itawezekana mkuu utusaidie hilo la kuongeza idadi ya polisi, wakiwa na gari la patrol, itakuwa imesaidia mambo matatu yafuatayo:

"La kwanza, itasaidia kutatua migogoro midogo midogo ya wakulima na wafugaji kwa sababu wenzetu wa Kenya wanaleta ng'ombe kwenye mashamba ya wakulima.

"Pili, itasaidia suala la wahamiaji haramu na tatu, itaziba ile mianya ya watu wanaokwepa kulipa kodi kwenye vituo halali vilivyopo Holili na Tarakea," alisema.

Akijibu ombi hilo, IGP Wambura alisema: "Mheshimiwa Mkuu wa Wilaya ameongelea suala la uhalifu katika eneo hili. Mimi na makamishna wangu tumepita tumeona hata jiografia jinsi tulivyokuja. Jiografia na ujirani wa hapa, bado unaona unahitaji kuwa na nguvu nzuri ya kukabili uhalifu uliotajwa na Mheshimiwa Mkuu wa Wilaya pamoja na aina nyingine za uhalifu ambao haukutajwa hapa.

"Kingine ni aina ya uhalifu. Nimekuja na Kamishna wa Polisi wa Kamisheni ya Polisi Jamii, Faustine Shilogile. Ninataka apate nafasi ya kuzungumza nanyi kuhusu nafasi ya jamii ya kukabiliana na uhalifu."

# Majeruhi 10 ajali iliyoua wahamishiwa Bugando

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

MAJERUHI 10 wa ajali ya basi lililogongana na lori aina ya fuso mkoani Shinyanga, wamehamishiwa Hospitali ya Rufani ya Kanda ya Ziwa (Bugando) jijini Mwanza kwa ajili ya kupatiwa matibabu zaidi.

Juzi watu watano walifariki huku 54 wakijeruhiwa katika ajali iliyohusisha basi na lori hilo katika eneo la Ibadakuli, Manispaa ya Shinyanga.

Ajali hiyo ilitokea majira ya saa nane usiku wakati basi hilo likitoka jijini Dar es Salaam kwenda jijini Mwanza. Akizungumza na Nipashe jana, Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Shinyanga, Dk. Luzila John, alisema kuwa baadhi ya majeruhi wa ajali hiyo wamehamishiwa Bugando jijini Mwanza kwa ajili ya kupatiwa matibabu zaidi.

Alisema kuwa kati ya majeruhi 54 ambao waliwapokea kutokana na ajali hiyo, 10 wamewapeleka Bugando kwa ajili ya kupatiwa matibabu zaidi, huku wengine wakiruhusiwa kuondoka baada ya kutibiwa na kwamba waliobaki hospitalini hapo ni majeruhi 14.

"Vifo katika ajali hii havijaongezeka, ila majeruhi 10 kati ya 54 ambao tuliwapokea, tumewapeleka Bugando jijini Mwanza kwa ajili ya kupatiwa matibabu zaidi kutokana na kuumia sana.

"Majeruhi wengine tuliwaruhusu kuondoka baada ya kuwapatia matibabu na tumesalia na majeruhi 14 katika hospitali yetu hapa Shinyanga, tunaendelea kuwapatia matibabu na wanaendelea vizuri," alifafanua.

Kaimu Kamanda wa Jeshi la Polisi Mkoa wa Shinyanga, Leonard Nyandahu, alisema chanzo cha ajali hiyo ni mwendokasi.

Alisema dereva wa basi hilo la kampuni ya Supernajimunisa lenye namba T.413 DAY hakuzingatia sheria za usalama barabarani na kutoa wito kwa madereva kufuata sheria hizo ili kuepuka ajali zisizo za lazima ambazo zinagharimu maisha ya watu.

# Ridhiwani aagiza usimamizi mpango matumizi ya ardhi

**Na Elizabeth Zaya**

NAIBU Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Ridhiwani Kikwete, amewataka viongozi wa Wilaya ya Handeni na Mkoa wa Tanga kwa ujumla kusimamia mipango ya matumizi bora ya ardhi katika maeneo yao ili kuepuka migogoro isiyo ya lazima.

Ridhiwani aliagiza hayo juzi wakati wa ziara ya Kamati ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii iliyotembelea Kijiji cha Msomera wilayani Handeni walikohamishiwa wananchi kutoka Hifadhi ya Ngorongoro na kupokea taarifa ya miradi ya ujenzi wa kijiji hicho.

"Zipo sheria ambazo zinasimamia mipango ya matumizi ya ardhi, kwamba mji kabla haujaanza kujengwa na kuendelezwa unapangwa kwa kuwekewa matumizi ya ardhi.

"Mfano, Kijiji cha Msomera tumepanga maeneo ya michezo, shule, hospitali, malisho, majosho ya wanyama, masoko na maeneo mengine ya umma na binafsi, hivyo ninawataka viongozi wa mkoa na wilaya msimamie matumizi hayo kikamilifu," aliagiza.

Ridhiwani alisema kuwa katika kijiji hicho, wizara ilipewa jukumu la kuandaa mpango wa matumizi ya ardhi ambapo mipango hiyo ilitakiwa kuendana na shughuli zitakazofanyika katika kijiji hicho.

Mkuu wa Mkoa wa Tanga, Omary Mgumba, akiwasilisha taarifa kwa Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge, Ally Makoa, alisema hadi Agosti 31 mwaka huu, walikuwa wamepokea jumla ya kaya 183 za wakazi wa Ngorongoro na kukabidhiwa nyumba 183 zenye jumla ya watu 1,056.

"Kazi ya kukabidhi nyumba linaenda sambamba na utoaji wa hati za hakimiliki za kimila katika viwanja na mashamba kwa kaya husika ambapo jumla ya hati za hakimiliki za kimila 355 zimetayarishwa na hati 176 ni kwa ajili ya makazi na za mashamba ni 179," alisema Mgumba.

Alisema kazi ya kuonyesha alama za mipaka ya viwanja na mashamba kwa kaya 183 zilizohamia kutoka Ngorongoro limekamilika na kila kaya imepatiwa ekari mbili na nusu za makazi pamoja na ekari tano za mashamba.

# ACT yawapitisha wawili kuwania ubunge EALA

**Na Elizabeth Zaya**

KAMATI Kuu ya Chama cha ACT-Wazalendo imewapitisha Ado Shaibu na Pavu Abdallah kuwania nafasi ya ubunge wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EALA) kwa tiketi ya chama hicho.

Uamuzi wa kuwapitisha Ado ambaye ni Katibu Mkuu wa chama hicho pamoja na mwenzake, ulifikiwa na Kamati Kuu ya chama hicho iliyoketi Septemba 2 na 3 mwaka huu jijini Dar es Salaam.

Ado alipitishwa kuwania nafasi hiyo kwa Tanzania Bara wakati Pavu kwa Zanzibar kuipeperusha bendera ya ACT-Wazalendo katika kinyang`anyiro hicho.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa kwa vyombo vya habari jana na Naibu Katibu wa Uenezi Habari, Janeth Rithe, wawakilishi hao wawili wa ACT-Wazalendo walipitishwa juzi na kamati hiyo.

Uchaguzi wa kuwapata wabunge wa EALA unatarajiwa kufanyika katika kikao kijacho cha Bunge ambacho wabunge wa Bunge la Tanzania watapiga kura na watakaoshinda, watakwenda kuiwakilisha Tanzania EALA.

Miongoni mwa vyama vilivyofanya mchakato wa kutoa nafasi kwa wanachama wake kujitokeza kuwania nafasi hiyo tangu dirisha la nafasi hiyo lilipofunguliwa ni Chama Cha Mapinduzi (CCM), ACT-Wazalendo na Chama cha Wananchi (CUF).

Rithe alisema Kamati Kuu ya ACT-Wazalendo pia ilifanya maandalizi ya ajenda za kikao cha Halmashauri Kuu ya chama hicho kilichofanyika jana Dar es Salaam.



Mkuu wa Wilaya ya Kongwa, Remidius Mwema, akizungumza na wakulima waliokabidhiwa matrekta ya mkopo yalitolewa na Kampuni ya PASS LEASING kwa ushirikiano na Kampuni ya Agro Com Company LTD katika hafla iliyofanyika juzi, Kibaigwa mkoani Dodoma, ambapo matrekta 15 yalikabidhiwa yenye thamani zaidi ya Sh. milioni 500. **PICHA: PAUL MABEJA**

# ...Mchujo makada 180 CCM waanza

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MCHUJO wa makada 178 wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), walioomba kuteuliwa kugombea Ubunge wa Bunge la Afrika Mashariki (EALA), ulianza jana na leo unaendelea chini ya Sekretarieti ya Halmashauri Kuu ya CCM Taifa.

Jana, Nipashe ilishuhudia makada hao wakiitwa mmoja baada ya mwingine kwenye kikao hicho katika moja ya kumbi zilizoko Ukumbi wa Mikutano wa Jakaya Kikwete jijini Dodoma.

Kwa mujibu wa taratibu za CCM, sekretarieti hiyo huketi chini ya Mwenyekiti wake ambaye ni Katibu Mkuu wa CCM na baada ya uhakiki wa nyaraka za wagombea, utafuata mchujo mwingine kwenye Kamati Kuu ya Halmashauri Kuu ya CCM Taifa (CC) na Kamati ya Wabunge wa CCM na uteuzi wa mwisho unatakiwa kufanywa na CC.

Hata hivyo, kwa mwaka 2017, utaratibu uliotumika baada ya wanachama 450 kujitokeza, wote walipelekwa kwenye kamati ya wabunge wa CCM ambapo walipigiwa kura kupata idadi iliyokuwa inatakiwa (sita). Hata hivyo, yalipelekwa majina ya wanachama 12 ili wapigiwe kura na Bunge ili ipatikane idadi inayotakiwa.

Katika Bunge la EALA, Tanzania inatakiwa kutoa wabunge tisa kupitia vyama vyenye uwakilishi bungeni.

CCM kupitia Katibu wa NEC, Idara ya Itikadi na Uenezi wa chama hicho, Shaka Hamdu Shaka (pichani), juzi ilitoa wito kwa wanachama hao kufika mbele ya kikao cha sekretarieti hiyo wakiwa na nyaraka zao zote muhimu zinazohusu sifa za kugombea nafasi hizo kwa ajili ya uhakiki na uratibu wa vikao



husika vya CCM.

"Kwa upande wa Tanzania Bara, kikao hicho kilifanyika jijini Dodoma jana na leo, kuanzia saa 3:00 asubuhi, hivyo kila mwombaji alitakiwa kufika Dodoma Septemba 3 mwaka huu ili kuitikia wito huo," alisema.

Hata hivyo, Shaka alisema kwa wagombea wa upande wa Zanzibar, nyaraka zao zitahakikiwa na kuratibiwa na kikao cha Kamati Maalum ya Halmashauri Kuu ya CCM ya Taifa, Zanzibar, kama itakavyoelekezwa na Naibu Katibu Mkuu wa CCM Zanzibar.

# Kilichowaokoa vigogo TRL kesi ukarabati mabehewa

**Na Grace Gurisha**

VIGOGO tisa wa Shirika la Reli Tanzania (TRL), akiwamo aliyekuwa Mkurugenzi Mtendaji, Kipalo Kisamfu, waliokuwa wanakabiliwa na mashtaka ya matumizi mabaya ya madaraka katika ununuzi wa mabehewa 25, wameachiwa huru na Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu.

Ilidaiwa kuwa Agosti 5, 2014, washtakiwa hao walitumia madaraka vibaya kwa kuidhinisha malipo ya dola za Marekani milioni 1.3 bila kuthibitisha matumizi ya mabehewa 25 kupitia cheti cha ukaguzi na cha kukubali kinachotolewa na TRL.

Mahakama hiyo ilifikia hatua hiyo mwishoni mwa wiki baada ya upande wa mashtaka kushindwa kuthibitisha mashtaka dhidi yao kutokana na ushahidi wao wa mashahidi zaidi ya 10 kuacha shaka. Akitoa uamuzi huo, Hakimu Mkazi Mkuu Huruma Shaidi, alisema kimsingi mahakama imeona ushahidi uliotolewa una shaka nyingi ambazo zinawasaidia washtakiwa.

Alisema kutokana na shaka hiyo, anawaachia huru washtakiwa wote kwa kuwa mwenye jukumu la msingi la kuthibitisha kesi bila kuacha shaka lolote ni upande wa mashtaka.

"Huu ndiyo uamuzi wa mahakama, ambaye hajaridhika akate rufani," alisema Hakimu Shaidi.

Hakimu huyo kwenye hukumu yake, alisema hakuna shahidi yeyote ambaye alitaja gharama ya marekebisho ya mabehewa hayo na pia hakuna faida yoyote waliyoipata washtakiwa.

Alisema iliyofanya kosa ni Benki ya Baroda Tanzania Ltd ambayo iliwalipa watu ambao siyo wahusika, ambapo iliwalipa asilimia 40 na asilimia 10 ya fedha hizo bila kuwapo na hati husika.

"Kwa hiyo, hakukuwa na faida waliyoipata washtakiwa, ushahidi upo wazi kwamba kama kulikuwapo na marekebisho ya mabehewa haya, basi yalifanywa na kampuni ile ile, tena kwenye kalakana ya TRL," alisema.

Mbali na Kisamfu, washtakiwa wengine ni Mkuu wa Kitengo cha Makenika na Mhasibu Mkuu, Jasper Kisiraga, Kaimu Meneja wa Usafiri, Mathias Massae, Kaimu Mhandisi wa Ufundi na Meneja Ujenzi, Muungano Kaupunda, na Mkuu wa Ufundi na Meneja Ujenzi, Ngoso Ngosomwiles.

Wengine ni Mhandisi Mkuu wa Ufundi, Paschal Mafikiri, Kaimu Mhandisi wa Mawasiliano, Felix Kashaingili, Mkuu wa Usafiri wa Reli, Lowland Simtengu, Mkuu wa Ubunifu na Utengenezaji wa Nyaraka, Joseph Syaizyagi na Kaimu Mkuu wa Usafirishaji, Charles Ndenge.

Katika tarehe tofauti kati ya Februari Mosi 2013 na Juni 30, 2014, katika Makao Makuu ya TRL, Kisamfu akiwa mfanyakazi wa mamlaka hiyo, alidaiwa kutumia vibaya madaraka yake kwa kushindwa kusimamia vizuri zabuni kama ilivyokuwa inatakiwa kwenye vigezo na masharti.

Inadaiwa kuwa jambo hilo ni kinyume cha Sheria Na. 21 ya Ununuzi ya 2004, jambo lililoipa faida Kampuni ya M/S Hindusthan Engineering and Industries Limited.

Ilidaiwa kuwa kati ya Julai Mosi na Agosti 31, 2013, Mafikiri alitumia madaraka yake vibaya kwa kuidhinisha michoro iliyoandaliwa na M/S Hindusthan, jambo ambalo ni kinyume cha vigezo na masharti ya zabuni.

Kaunda pia alidaiwa kutumia madaraka vibaya kwa kuruhusu kutengenezwa kwa mabehewa 25 bila kuzingatia vigezo na masharti ya zabuni hiyo.

Katika mashtaka yanayowakabili Kaupunda, Mapunda, Kashaigili, Simtenguna Syaizyagi, ilidaiwa kuwa kati ya Januari Mosi na Februari 2014, wakiwa wajumbe wa bodi ya zabuni hiyo, walitumia madaraka yao vibaya kwa kuiruhusu M/S Hindusthan kushinda, ilhali haikukidhi vigezo vya kupewa zabuni hiyo.


JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
MAHAKAMA YA TANZANIA
KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO YA WILAYA YA MBEYA
KITUO CHA MJINI MKOA WA MBEYA
USIMAMIZI WA MIRATHI Na. 99/2022
KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA
MAREHEMU STEVEN YAKONYA MPENZU WA MSHEWE
KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI
YALIYOLETWA NA JULIUS LASTON MPENZU

**TANGAZO**

*(Kanuni ya 5(2) ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi katika Mahakama za Mwanzo)*

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 13 Mwezi 07 Mwaka 2022 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

**Zingatia;** Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.
**Imetolewa leo tarehe 04 Mwezi 7 Mwaka 2022.**

HAKIMU



## KUPOTEA KWA VYETI



**GODBLESS JUDICA SWAI** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S.0479/0035** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **NRONGA** Sekondari mwaka 1999. Cheti cha kidato cha sita chenye index namba **S.0356/0527** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **VUNJO SEKONDARI** mwaka **2002.** Yeyote atakayeviona atoe taarifa kituo cha polisi.
**Taarifa ya polisi: DAR/KIL/RB/334171 /2022.**



## KUPOTEA KWA OFA YA KIWANJA

**Enock Tambalu Bunango**
Anatangaza kupotelewa na Ofa ya kiwanja namba 400 kitalu "NN" kilichopo Ndala Manispaa ya Shinyanga.
Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo cha Polisi kilichopo karibu au awasiliane na Enock Tambalu Bunango kwa simu **0684283787**
**Rbnamba/SHI/SHI/RB/224412/2022**

JACOB F. MWINUKA
AFISA ARDHI
MANISPAA SHINYANGA

AFISA ARDHI WA MANISPAA SHINYANGA



## KUPOTELEWA NA NYARAKA YA UMILIKI WA KIWANJA

**Crethensia Misango**
Anatangaza kupotelewa na nyaraka ya umiliki kiwanja **namba 81 kitalu "mm"** kilichopo Lubaga Manispaa ya Shinyanga.
Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo cha Polisi kilichopo karibu au awasiliane na Crethensia Misango kwa simu namba **0716159113**
**Rbnamba;**
**DSM/PHQ/RB/347288/2022**

MUNICIPAL LAND OFFICER SHINYANGA
Musa Makungu
AFISA ARDHI
MANISPAA YA SHINYANGA

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Wawakilishi wetu CAF malizeni kazi mapema

**WAWAKILISHI** wa Tanzania Bara kwenye michuano ya kimataifa kwa upande wa klabu, Simba, Yanga na Geita Gold Jumamosi na Jumapili wiki hii, watashuka katika viwanja tofauti ndani na nje ya nchi kuanza kuwania kupeperusha vema bendera ya Tanzania kwenye Ligi ya Mabingwa na Kombe la Shirikisho Afrika.

Simba na Yanga zinaiwakilisha nchi kwenye Ligi ya Mabingwa wakati Geita Gold na Azam FC ambayo yenyewe itaanzia raundi ya kwanza, zikiwa na jukumu la kuipeperusha vema bendera ya taifa kwenye Kombe la Shirikisho Afrika. Kwa upande wa Simba, itaanzia ugenini Jumamosi wiki hii dhidi ya Nyasa Bigi Bullets ya Malawi, wakati Yanga yenyewe ikiangukia bahati ya mtende baada ya Zalan FC ya Sudan Kusini, kuomba mechi zake zote mbili kuchezwa hapa nchini katika Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Zalan FC ambayo mchezo wa Jumamosi itakuwa mwenyeji, imeomba kuutumia Uwanja wa Benjamin Mkapa kutoka na hali ya usalama nchini kwao kutokuwa shwari.

Kwenye Kombe la Shirikisho, Geita Gold itaanzia ugenini nchini Sudan dhidi ya wenyeji wao, Hilal Alsahil, katika mchezo utakaopigwa Jumapili wiki hii kabla ya timu hizo kurudiana nchini Jumamosi ya juma lijalo.

Kwa ujumla michuano hii inahitaji mahesabu makali kwa kila timu kuchanga karata zake vizuri ili kuweza kuvuka hatua hii ya awali kwenda raundi ya kwanza ambayo kwa timu zinazoshiriki Ligi ya Mabingwa zitakuwa na faida kubwa ya kuweza kuendelea kuchuana kimataifa hata zikipoteza. Hii ni kutokana na kanuni ya mashindano hayo, kutoa faida kwa timu zinazoshiriki Ligi ya Mabingwa ambazo zitatolewa katika raundi ya kwanza (baada ya hii ya awali), huangukia kwenye mechi za mchujo za Kombe la Shirikisho na zikishinda hutinga hatua ya makundi ya michuano hiyo ya pili kwa utajiri kwa ngazi za klabu barani Afrika.

Hivyo, kinachotakiwa kwanza ni Simba na Yanga kuelekeza malengo yao kwenye kuendelea kushiriki Ligi ya Mabingwa kwa kuhakikisha zinafanya vizuri kwenye mechi zao za awali ugenini kwa kupata ushindi mnono ili kurahisisha kazi katika michezo yao ya marudiano mwishoni mwa wiki ijayo. Tunatambua si kazi rahisi kwa kuwa timu zote zilizotinga hatua hiyo ni zile zilizofanya vizuri kwenye ligi zao za ndani, lakini kutokana na usajili wa maana wa klabu zetu hadi maandalizi zilizofanya, tunaamini hakuna kinachoshindikana kama kila mmoja kwa nafasi yake atajitoa kikamilifu kutekeleza majukumu yake kuanzia viongozi wa timu hizo, mabenchi ya ufundi, wachezaji hadi mashabiki. Wakati huu ambao barani Afrika bado kanuni ya timu kufaidika kwa bao la ugenini ikitumika, ni wakati muafaka kwa wawakilishi wetu hao wa nchi kuitumia vema katika mechi zao hususan ni raundi hii ya awali ambayo zote zinaanzia ugenini.

Kinachotakiwa ni kuhakikisha yanapatikana mabao mengi na kutokubali kuruhusu nyavu zao kutingishwa ili michezo ya marudiano hata kama zikiambulia sare ya aina yoyote ile, ziwe na uhakika wa kutinga raundi ya kwanza. Lakini katika kufanikisha hilo, ni wakati wa mashabiki kujitoa bega kwa bega kuongozana na timu zao ugenini kwenda kuzipa sapoti kwani tunaamini siku zote shabiki wa soka ni sawa na mchezaji wa 12 uwanjani, pale anapojitokeza kuishangilia mwanzo mwisho.


Kwa hatua hii ya awali ambayo Simba na Geita Gold FC zitakuwa ugenini, tunaamini kwa mashabiki kujipanga kwenda Malawi ama Sudan, wanaweza kabisa kumudu gharama hizo, jambo ambalo litaonyesha mapenzi makubwa na nia ya dhati ya kuziunga mkono klabu zetu.

Lakini kwa mashabiki wa Yanga na Watanzania kwa ujumla, huu ni wakati wa kujitokeza kwa wingi katika Uwanja wa Benjamin Mkapa kuipa sapoti klabu hiyo katika michezo miwili itakayocheza nchini dhidi ya Zalan FC.

Tunatambua wapo ambao wanaweza kuibeza Zalan FC kwa kuiona ni timu ya kawaida kutokana na nchi inayotoka kuwa chini kisoka ukilinganisha na Tanzania, jambo ambalo hatuna budi kuwaonya wachezaji wa Yanga na benchi la ufundi kwa kutoichukulia 'poa' timu hiyo kwa kuwa siku zote mchezo wa soka huwa na matokeo ya kushangaza.

Hivyo, kwa muda huu wa siku takriban nne zilizobaki kabla ya mitanange hiyo kupigwa, tunawatakia maandalizi mema wawakilishi wetu, lakini tukiamini makocha watatumia muda mfupi kuziba panapovuja na kuwajenga zaidi wachezaji wao kisaikolojia.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






Na Adam Fungamwango

## Muungwana Lazima Nilonge

# Kipigo Stars kila mtu abebe lawama

**SAFARI** ya Tanzania kusaka tiketi ya kufuzu fainali za Mataifa ya Afrika kwa Wachezaji Wanaocheza Ligi za Ndani (CHAN), ilimalizika juzi kwenye Uwanja wa St Mary Chitende kwa kuchapwa mabao 3-0 dhidi ya timu ya Taifa ya Uganda, The Cranes.

Taifa Stars baada ya kufungwa bao 1-0 kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa Agosti 28, mwaka huu, juzi ilikubali tena kipigo cha 3-0 hivyo kutolewa kwa jumla ya mabao 4-0 na kuwaacha wenyeji wakifuzu fainali hizo zitakazofanyika mwakani nchini nchini Algeria.

Pamoja na kutimua benchi lake la ufundi lililokuwa likiongozwa na Kim Poulsen, bado haikuwa na ubavu dhidi ya kikosi cha Uganda Cranes licha ya kuwa na kocha mpya, Honour Janza na Msaidizi wake, Mecky Maxime.

Mara ya mwisho ilikuwa mwaka 2019 ilipokata tiketi ikiwa ugenini Uwanja wa Omdurman nchini Sudan ilipowafunga wenyeji mabao 2-1, licha ya kufungwa bao 1-0 nchini ikafuzu kwa bao la ugenini kutokana na matokeo ya jumla kuwa mabao 2-2, ikiwa chini ya kocha Mrundi Etienne Ndayiragije na kucheza fainali hizo zilizofanyika nchini Cameroon 2020.

Kila Mtanzania amekuwa na maoni tofauti juu ya kipigo hicho ambacho hakikutarajiwa. Inawezekana ikawa Stars ingeweza kutolewa, lakini kwa jumla ya mabao 4-0, hivyo kuzua mjadala mkubwa sehemu mbalimbali nchini, vyombo vya habari na mitandao ya kijamii.

Awali ilipofungwa bao 1-0, ilikuwa rahisi tu kumnyooshea kidole kocha Poulsen, ikidaiwa yeye ndiye sababu kwani ameishiwa mbinu. Na wengi walidhani hivyo, ikiwamo baadhi ya wachambuzi. Baada ya mabao 3-0 hali imebadilika, hivi sasa kama kawaida ya Watanzania kila mmoja anatafuta mtu wa kumbebesha lawama. Siyo Poulsen tena, kwa sababu hayupo. Nadhani kama asingetimuliwa, jumba bovu lingezidi kumwangukia yeye na ilikuwa ndiyo atimuwe, huku kila mmoja akimimina tatizo lilikuwa yeye.

Hii si mara ya kwanza kwa Stars kufungwa kwenye michuano mbalimbali ya kimataifa. Stars imekuwa ikifuzu AFCON na CHAN unaweza kusema kibahati zaidi kuliko uhalisia wenyewe.

Ndiyo maana haijawahi kufuzu kwa kuongoza kundi. Wapo wanaolilaumu Shirikisho la Soka nchini (TFF), kwa sababu zao wanazozijua, wengine wakilaumu kuwapo kwa wachezaji 12 wa kigeni kwenye Ligi Kuu kuwa eti ndiyo inasababisha kusiwe na wachezaji wenye uwezo Stars, lakini wapo wanaolaumu moja kwa moja wachezaji.

Binafsi nasema kuwa kutofanya vema kwa Stars kila Mtanzania anastahili kubeba lawama, kwa sababu kushindwa huko kunaanzia mbali sana.

Wanaosema ni kwa sababu ya kuwapo kwa ruhusa ya wachezaji 12 wa kigeni kwenye Ligi Kuu kwa kila timu, inafaa aulizwe kwa nini wachezaji wa Kitanzania wao hawaendi nje ya nchi, na ikichaguliwa wawe wanatoka huko, huku Ligi Kuu ya Tanzania kukiwa na wachezaji wachache?

Na kama ni CHAN ambayo ni ya wachezaji wa ndani tu, kwani ni lazima wote watoke Simba, Yanga au Azam ambao wana uwezo wa kusajili idadi hiyo ya wachezaji?

Mbona timu ya Taifa ya Uganda wachezaji waliotunyanyasa wao wengi wametoka kwenye klabu ndogo tu za Vipers, Wakiso Giants, URA, KCCA, Proline, BUL FC, Onduparaka, Arua Hill na mmoja tu kutoka klabu kubwa za Express na watatu tu SC Villa.

Wenzetu wanaangalia uwezo kwa wakati huo na si kukariri majina ya wachezaji wa klabu kubwa kama Express na SC Villa.

Hapa Tanzania wachezaji wanachaguliwa kisiasa zaidi kuliko uwezo. Wakati Uganda ikiwa na wachezaji ambao misimu michache iliyopita walicheza mechi za vijana chini ya miaka 17, Stars ilikuwa na John Bocco ambaye ana zaidi ya miaka 10 kwenye Ligi Kuu.

Na Bocco anachukuliwa kutokana na hawa wachezaji wetu vijana wanakuwa hawana mwendelezo wa viwango vyao. Wengi wanakuwa mastaa wa msimu mmoja au miwili tu, matokeo yake hadi leo tunakuwa na wachezaji wale wale tu.

Hapa kuna sehemu tunakosea, na tuanzie chini kabisa, kwenye kutengeneza vijana hakuna makocha sahihi kwani mpaka leo wanafundishwa kupokea pasi, malezi kutoka kwa baadhi ya wazazi, kutokuwa na viwanja vya michezo ambavyo vingi kwa sasa vimegeuzwa gereji baada ya kupigwa bei na mamlaka husika, pamoja na mtindo wa maisha ya kisasa kwa wachezaji wetu yanawafanya wawe na matatizo mengi.

Ukitaka kujua matatizo ya wachezaji wa Kitanzania wawe peke yao kwenye timu moja kama hivyo Stars, utagundua mengi tofauti wakichanganyika na wachezaji wa nje ya nchi ambao huwa wanawafichia makosa.

Hii inaonyesha kuwa tatizo la Stars ni mtambuka, halikuanza kufungwa leo au jana, kila mtu abebe mzigo wake. Hakuna wa kumlaumu mwenzake mpaka hapo, hadi Watanzania wote tutakapoanza kubadilika.



Mwongoza watalii wa Kampuni ya Utalii ya ZARA Tanzania Adventures ya mjini Moshi, Faustine Chombo (kushoto), akiwaongoza watalii katika kilele cha Mlima Kilimanjaro cha Uhuru Peak (5,895m ASL) katika eneo la Stella Point (5 ,685m ASL) juzi. **PICHA: JAMES LANKA**

# EPZA, CPB zasaini hati ushirikiano kibiashara

**Na Mwandishi Wetu**

MAMLAKA ya maeneo maalum ya uwekezaji kwa mauzo ya nje (EPZA) imesaini hati ya ushirikiano wa kibiashara na Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko (CPB) katika uwekezaji nchini.

Mkurugenzi Mkuu wa EPZA, Charles Itembe, akizungumza wakati wa utiaji saini huo, alisema, huo ni mwanzo kati ya mambo mengi ambayo taasisi hizo zimeyajadili katika uwekezaji.

"Yapo maeneo mengi sana ambayo taasisi hizi zinaweza kushirikiana, lakini kwa kuanzia na ukizingatia kwamba EPZA hivi karibuni ilikabidhiwa viwanda vinane na Msajili wa Hazina ambavyo ubinafsishaji wake haukufanikiwa kutafuta wawekezaji ili kuvifufua na kuviendeleza tena na kufanya kazi iliyokusudiwa ili taifa liweze kufaidika na ajira na uuzaji wa bidhaa zilizoongezwa thamani," alisema.

Alisema katika ushirikiano huo wa kibiashara, utaanza na kiwanda cha kubangua korosho kilichoko Wilaya ya Nachingwea mkoani Lindi.

"CPB wamebobea sana katika shughuli hizi za uwekezaji katika kilimo na ni taasisi ya umma na kwa bahati kwamba zote kama taasisi za umma zinaweza kufanya uwekezaji. CPB wana uwezo wa kuwekeza na wamefanya upembuzi yakinifu wa kina kuona namna gani wanaweza kukifanya kiwanda hiki cha kubangua korosho cha Nachingwea kuwa cha kisasa na kuongeza thamani katika korosho ili kupata bei ya juu katika soko," alisema.

Alisema makubaliano hayo yanalenga kuangalia njia bora zaidi ya taasisi hizo mbili za serikali kufanya kazi pamoja, CPB kama mwekezaji katika maeneo maalum ya kiuchumi yaliyo chini ya EPZA.

Pia Mamlaka ya EPZA kama taasisi yenye mamlaka ya kusimamia uwekezaji unaofuata sera za uwekezaji katika maeneo maalum ya kiuchumi kadiri ya sheria iliyoianzisha.

"CPB imekuwa ya kwanza kuona fursa na mstari wa mbele kuifanyia kazi hasa baada ya kufanya upembuzi yakinifu wa kina wa kuwekeza katika kiwanda cha kubangua korosho cha Nachingwea," alisema.

Kwa mujibu wa EPZA kiwanda hicho kwa sasa kinatumiwa na Halmashauri ya Wilaya ya Nachingwea kwa ajili ya kuhifadhi korosho. Lakini CPB itakitumia pia kubangua na kuongeza thamani ya korosho ili kupata bei kubwa katika soko la dunia ikizingatiwa Tanzania ina viwanda vichache vya kubangua na kuongeza thamani ya zao la korosho.

Pia ukosefu wa viwanda vya kutosha vya kubangua korosho kunaikosesha nchi fedha za kigeni. "Kwa uwekezaji huu wa CPB, nchi itapata fedha nyingi za kigeni, ajira nyingi zitazalishwa na kusukuma mbele uchumi wa nchi."

Mkurugenzi Mkuu wa CPB, Dk. Anselm Moshi alisema kiwanda hicho cha kubangua korosho kitakuwa na uwezo wa kuchakata tani 10,000 kwa mwaka.

"Huu ni mwanzo tu wa utekelezaji wa makubaliano yetu ukiwa na lengo la kuiongezea thamani ya korosho yetu ili kupata bei kubwa katika soko la dunia," alisema.

Alisema tahadhari zote muhimu zimechukuliwa katika kufufua na kuendeleza kiwanda hicho ili kufanya uchakataji wa korosho kuwa endelevu na kuepuka kuanguka katika mtego uliofanya uwekezaji wa mwanzo kushindwa na kiwanda kufa.

# Ujenzi nyumba Kawe kuendelea Novemba

**Na Elizabeth Zaya**

TAASISI ya Nyumba za Watumishi (WHI) inatarajia kuanza utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa nyumba katika eneo la Kawe jijini Dar es Salaam, Novemba mwaka huu.

Akizungumza na Nipashe jana, Ofisa Uhusiano na Mawasiliano wa kampuni hiyo, Maryjane Makawia, alisema ujenzi katika mradi huo unatarajiwa kutumia mwaka mmoja hadi miwili.

"Watumishi Housing Investments kwa mwaka huu wa fedha 2022/23 tumepanga kutekeleza mradi wa Kawe Apartment, lengo likiwa ni kuhakikisha kuwa Watanzania wanapata makazi bora kwa bei nafuu. Tumepata eneo lenye ukubwa wa ekari 10 ambapo kwa sasa kilichobaki ni michoro na ramani ili mradi uanze," alisema Makawia.

Alisema zaidi ya nyumba 1,000 zinatarajiwa kujengwa katika mradi huo.

"Utaratibu wa kulipia utakuwa ule ule ambao umekuwa ukitumika katika miradi yetu iliyotangulia ikiwamo kulipia manunuzi ya nyumba kidogo kidogo wakati inajengwa na baada ya kukamilika. Pia kutatolewa fursa kwa wananchi kupanga," alisema Makawia.

"Ndiyo maana utaona hata kwenye mradi wetu wa Gezaulole tuna nyumba za kupanga kwenye maghorofa ili kusaidia wale ambao wanahitaji kupanga nyumba nzuri."

Pia Makawia alisema wanatarajia kuanza mradi wa kuuza viwanja katika eneo la USA-River jijini Arusha, mradi wa nyumba Dodoma katika eneo la Mtumba na Chamwino, pamoja na jengo la biashara Kigamboni.

Kadhalika, wanatarajia kuanza mradi mwingine wa ujenzi wa nyumba za makazi Kigamboni.

Januri 18, mwaka huu serikali kupitia kwa Waziri wa Nchi Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Jenista Mhagama, aliitaka WHI kuongeza ubunifu ikiwamo kukuza mtaji wake ili kutekeleza miradi mingi zaidi itakayosaidia watumishi wa umma.

Alisema mahitaji ya nyumba za watumishi nchini ni milioni tatu na kwamba uhitaji wa nyumba kwa watumishi hao ni 200,000 kila mwaka.

Julai 27, mwaka huu, Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angeline Mabula, akizungumza katika mkutano mkuu wa 41 wa Taasisi ya Shelter Afrique mjini Victoria Falls nchini Zimbabwe, alisema kuwa Tanzania imepiga hatua katika utoaji mikopo ya nyumba na jumla ya mikopo 6,182 ilikuwa imetolewa katika mwezi huo, ikilinganishwa na mikopo 579 iliyotolewa mwaka 2009.

Dk. Mabula alisema muda wa urejeshaji mikopo umeongezeka kutoka miaka 15 hadi 25 huku riba ya mkopo ikipungua kutoka asilimia 20 hadi 22 mwaka 2009 na kufikia asilimia 15 hadi 19 inayotozwa.

# Serikali yavimulika vikwazo vya mamantilie

**Na Halfani Chusi**

WAZIRI wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Dk. Dorothy Gwajima, amewataka wanawake wote wanaojishughulisha na biashara ya uuzaji wa chakula maarufu mamantilie, kupika chakula kwa kuzingatia usafi na lishe.

Aliagiza hayo juzi jijini Dar es Salaam wakati wa Tamasha la Mamantilie na kuahidi kutatua vikwazo vinavyowakabili, ikiwamo kuwa na maeneo rasmi ya kufanyia biashara ili kuepuka bughudha.

Alisema mamantilie wanapaswa kujengewa mazingira mazuri na kutatuliwa vikwazo ili kupitia kazi hiyo wapate kipato kikubwa na kumudu kutoa huduma kwa familia zao. "Mamantilie ni kazi ambayo wanawake wengi wanafanya na wamejiajiri, tunambua michango yao katika urahisishaji wa upatikanaji wa chakula, watoa huduma hii wanapaswa kuzingatia sifa na vigezo vyote na serikali ipo tayari kuwasaidia.

"Kwa kuona umuhimu wa mamantilie na vikwazo wanavyopitia, Rais Samia Suluhu Hassan katika wizara yangu alitafakari na kuongeza kundi la mamantilie. Kwa hiyo, hizi shida nitazifikisha na hili la kutaka kutambuliwa kisera, halina ubishi na uzuri tupo kwenye mapitio ya sera, kwa hiyo utakapofikia muda wa kulijadili hilo, tutawashirikisha ili tuzungumze pamoja. "Mmeongelea pia shida ya ufadhili na mikopo nafuu, tumeipokea, mikopo ipo, lakini lazima tukae pamoja tuone namna ya kuwakopesha," alisema.

Waziri huyo pia alibainisha kuwa mamantilie waliokuwa wamekusanyika eneo hilo mikakati iliyowekwa na serikali kwa ajili ya kuwainua wanawake wajasiriamali kiuchumi.

"Kwanza, huwa tunayo mikopo kwa ajili ya wanawake na watu wenye ulemavu ambayo chanzo chake ni ile asilimia 10 ya mapato ya ndani ya halmashauri husika, na kama katika mikopo hii kuna mamantilie hakupewa, tutapita mimi na jopo langu, mamlaka zote kuona fedha ilipotelea wapi.

Aliwahimiza wanawake kutobaki nyuma hasa kwenye makongamano ya siku za wanawake duniani, akibainisha kuwa hiyo ndiyo sehemu ya kupeleka malalamiko yao.

"Sabasaba itakayokuja mwakani lazima muwapo muonyeshe shughuli zenu watu wazifahamu kwa ukubwa wake, pia muwe mnahudhuria makongamano ya kimataifa ya wanawake, kule huwa zinaibuka fursa nyingi na mtapata nafasi ya kuwasilisha shida zenu," alisistiza.

Katika tamasha hilo, Dk. Dorothy aliwataka wanawake kutoa ushirikiano kwa kutoa taarifa zinazohusisha ukatili wa kijinsia kwa kupiga namba 119 bila malipo.

Mkurugenzi wa Wanawake Jikoni Business, Nice Mamuya, alitaja vikwazo ambavyo vinawakabili mamantilie huku akiomba serikali kufanya hima kuvitatua.

"Mamantilie tunakabiliwa na vikwazo vingi, kukosa maeneo sahihi kwa ajili ya kufanyia biashara, mitaji midogo kwa wafanyabiashara, kuondolewa sehemu tulizokuwa tukifanyia biashara na kupelekwa sehemu ambazo hazina wateja, pamoja na kukosa bima na ufadhili kutoka kwa wadau wa maendeleo," aliwasilisha.

Mwajuma Musa, mmoja wa mamantilie aliyehudhuria katika tamasha hilo, alisema amefurahi kusikia mikakati mizuri ambayo imewekwa kwa ajili ya kuwainua wanawake hasa mamantilie.

# Trafiki wabaini shida mabasi ya wanafunzi

**Na Samson Chacha,** TARIME

WAKATI shule zikifunguliwa leo, Kikosi cha Usalama Barabarani Mkoa wa Kipolisi Tarime Rorya kimefanya ukaguzi wa mabasi yanayobeba wanafunzi na kukuta baadhi yana makosa.

Makosa yaliyobainika juzi katika ukaguzi huo ni baadhi ya magari kukutwa na makosa yakiwamo kutokuwa na mikanda katika viti, pia uchakavu.

Kaimu Mkuu wa Kikosi cha Usalama Barabarani Mkoa wa Kipolisi Tarime, Peter Mtali, alitoa wito kwa wamiliki wa shule kupeleka magari yao ili yakaguliwe, vinginevyo yatafungiwa kubeba wanafunzi.

Mtali alifanya ukaguzi kwa kushirikiana na Sajenti Abdalah ambaye ni Mkaguzi Magari na Koplo Maxmillian ambaye ni Mtoa Elimu na Mafunzo ya Usalama Barabarani Wilaya za Tarime na Rorya.

"Tumeanza ukaguzi wa magari yanayobeba wanafunzi kwa awamu ya pili kabla shule hazijafunguliwa Jumatatu (leo), mwishoni mwa mwezi Julai mwaka huu, tulifanya ukaguzi wa awamu ya kwanza na baadhi yalikutwa na makosa yakiwa mabovu kutokuwa na mikanda kwenye viti, vioo kupasuka, matairi kuchakaa, injini na gia boksi zilikuwa mbovu na mengine breki zilikuwa hazifanyi kazi vizuri," alisema.

Kiongozi huyo alisema ukaguzi huo unahusisha magari yote yanayobeba wanafunzi katika wilaya za mkoa huo.

Alisema katika ukaguzi huo yapo magari ambayo wameyaondolea namba zake ili makosa yaliyokutwa nayo yakarekebishwe. "Wale wote ambao hawajaleta magari yao kufanyiwa ukagauzi, wanatakiwa kuleta, tulishatoa matangazo na watakaokaidi agizo hili na kuendelea kubeba wanafunzi wakati hawajakaguliwa, hatua kali zitachukuliwa dhidi yao zikiwamo kuwafikisha mahakamani," alisema.

Mtali alitaja baadhi ya mabasi ya shule yanayotakiwa kukaguliwa ni ya St. Jude, Nyangoto, St. Magreth, Moregas, Mwera Vission, Helgaton, Engel, Bustani, Odikwa, Eamanuel King, Baraton, St. Luka, Riders, Pop Paulo, Bwire, Masiaga, Modester Rehema na St. Agustino.




Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Dk. Dorothy Gwajima (wa pili kulia), akiangalia kazi za wajasiriamali, alipohudhuria tamasha la mama ntilie, viwanja vya Leaders Club jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Vibanda vya machinga vilivyoteketea kwa moto

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

VIBANDA zaidi ya 50 vya wafanyabiashara wadogo, maarufu machinga, na mama lishe vilivyoko Kata ya Ipembe Manispaa ya Singida vimeteketea kwa moto.

Akizungumza na waandishi wa habari jana, Mkuu wa Wilaya ya Singida, Paskas Mragili, alisema tukio hilo lilitokea usiku wa kuamkia jana na moto kuteketeza vibanda hivyo ambavyo ni kati ya 100 vilivyoko eneo hilo.

Alisema eneo hilo lilikuwa linatumiwa na machinga kwa ajili ya kuuza nguo, viatu na bidhaa mbalimbali pamoja na mama lishe kutoa huduma kwa wateja.

Muragili alisema chanzo cha tukio hilo ni kijana mmoja ambaye alikuwa akifanya ukarabati wa kibanda chake kwa kuchomelea, baadaye zilitokea cheche na moto kuzuka na kuanza kuviteketeza vibanda hivyo.

Alisema kuwa kama kijana huyo angetoa taarifa mapema kwa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji baada ya tukio kutokea, madhara yasingekuwa makubwa. Hivyo, alitoa wito kwa wananchi wanapofanya kazi kama hizo za kuchomelea vyuma nyakati za usiku, iwe nyumbani au viwandani, wachukue tahadhari. Muragili alisema kuwa kutokana na tukio hilo, Kamati ya Ulinzi na Usalama chini ya Mkuu wa Mkoa wa Singida, Peter Serukamba, itakaa na kufanya tathmini ya hasara iliyopatikana na serikali itatoa taarifa rasmi.

Mkuu wa Mkoa Singida, Peter Serukamba, alisema wafanyabiashara wamepata hasara kutokana na uzembe uliosababisha na mtu mmoja aliyekuwa akichomelea vyuma kwenye kibanda chake.

Alisema: "Ni jambo kubwa la masikitiko, tunawapa pole wafanyabiashara kwa tukio hili lililotokea, serikali itachunguza kwa kina na kuchukua hatua."

Mwenyekiti wa Wajasiriamali Manispaa ya Singida, Mohammed Swalehe, alisema wafanyabiashara wamepata hasara kubwa kutoka na kuzuka kwa moto huo.

Kamanda wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji Mkoa wa Singida, Devotha Bigawa, alisema kuwa baada ya kupata taarifa na kufika eneo la tukio, walichokifanya ni kuzuia mto usilete madhara maeneo mengineyo ikiwamo Hospitali ya Mkoa, Shirika la Posta na tangi la mafuta.

Bigawa alisema tatizo walilokutana nalo wakati wa kuzima moto huo ni miundombinu, kwamba hakukuwa na sehemu ya kupitishia gari kutokana na namna vibanda hivyo vilivyojengwa.

# ASA yachimba visima vya umwagiliaji Kilosa

**Na Renatha Msungu,** KILOSA

WAKALA wa Mbegu za Kilimo Tanzania (ASA) umeanza kutekeleza agizo la serikali la kuweka miundombinu ya kisasa ya umwagiliaji katika mashamba yake ya uzalishaji wa mbegu kwa kuchimba visima vitatu.

Akizungumza na waandishi wa habari juzi, Mtendaji Mkuu wa ASA, Dk. Sophia Kashenge, alisema visima hivyo vitaunganishwa na mitambo ya umwagiliaji katika shamba la uzalishaji mbegu la Msimba lililoko wilayani Kilosa mkoani Morogoro lenye zaidi ya ekari 300.

Alisema hadi sasa shamba la Msimba tayari lina visima vitatu virefu ambavyo vyote vina toa maji kwa uhakika, hali ambayo itawezesha umwagiliaji wa kisasa baada ya kufungwa kwa mitambo hiyo ya umwagiliaji.

Dk. Kashenge alisema ASA imeanza kufunga miundombinu ya umwagiliaji katika shamba hilo na utahusisha mashamba mengine ambayo yatafungiwa kwa vipindi tofauti.

"Uzalisha wa mbegu ni kipaumbele chetu, tumepewa maagizo na Wizara ya Kilimo ya kuhakikisha ndani ya muda mfupi katika mashamba yetu tuweke miundombinu ya umwagiliaji na hili tumelianza," alisema.

Dk. Kashenge alisema mkakati wa wakala ni kuongeza uzalishaji wa mbegu za alizeti kwa maelekezo ya wizara ambapo kwa sasa uzalishaji ni zaidi ya tani 1,000 huku malengo kwa mwaka, ujao ni tani 5,000 za mbegu za alizeti katika mashamba yote ya mbegu yanayomilikiwa na ASA.

Alitaja mashamba mengine ambayo yatawekewa miundombinu ya umwagiliaji kwa mwaka huu wa fedha ni pamoja na shamba la Mwele (Tanga), Ngara Mtoni (Arusha) pamoja na shamba la Kilimi mkoani Tabora na lengo ni kufikia takribani ekari 10, 000.

Mbunge wa Kilosa, Prof. Palamagamba Kabudi, alisema ASA wameanza kupiga hatua kubwa za uzalishaji wa mbegu hasa kwa kuanza kuweka mifumo hiyo ya umwagiliaji Morogoro.

Alisema serikali inatekeleza mapinduzi makubwa katika sekta ya kilimo hususani kwa lengo la kuacha kutegemea kilimo cha mvua na kufanya kile cha kisasa cha umwagiliaji kinachokabiliana na janga la mabadiliko ya tabia nchi.

Prof. Kabudi alisema bajeti ya Wizara ya Kilimo kwa mwaka huu wa fedha, 2022/23 imeongezwa kutoka Sh. bilioni 200 hadi Sh. bilioni 900 ili kuchochea ufanisi wa utafiti na uzalishaji wa mbegu nchi hususani mbegu za alizeti.

Alisema hatua ya kuwekwa miundombinu katika shamba hilo itaongeza tija ya uzalishaji wa mbegu kwa wingi na kuifanya nchi iweze kujitegemea na hata kuziuza nchi za jirani.

Katika hafla hiyo, duka la ASA la kuuza mbegu kwa wananchi katika Wilaya ya Kilosa lilizinduliwa ili kuwarahisishia wananchi kuzinunua badala ya kutembea umbali mrefu kuzitafuta.

HABARI KITAIFA

## Wajinyakulia pikipiki kwa kuweka akiba benki

**Na Frank Monyo**

BENKI ya NCBA imekabidhi zawadi ya pikipiki tatu kwa washindi wa awali wa kampeni ya Mpawa ijulikanayo 'chuzi limekubali' iliyoanza mwezi Agosti, mwaka huu katika viwanja vya soko la Mabibo.

Kampeni hio inafanywa kwa ushirikiano na Kampuni ya Simu ya Vodacom ambayo imelenga kuwahamasisha Watanzania kuweka akiba ili kujihakikishia fedha zaidi katika akaunti zao.

Kwa mujibu wa msimamizi wa kitengo cha fedha kutoka NCBA, Genesi Kunda, huduma ya Mpawa imekuwa mstari wa mbele kuwasaidia Watanzania kwa muda mrefu kupata mikopo ya haraka na kwa riba nafuu.

"Kampeni hii imelenga kuhamasisha wateja wetu na Watanzania kwa ujumla kuweka akiba ya fedha zao kupitia huduma ya Mpawa ambapo pia wataweza kupata mikopo ya haraka na kwa riba nafuu kuliko sehemu au huduma zingine zozote," alisema Kunda.

"Tunatoa fedha taslimu Sh. 50,000 kwa wateja wanaorejesha mikopo yao ndani ya siku sita. Kila wiki kuanzia wiki hii tumewazadia wateja 50 waliorejesha mikopo yao mapema na kuweka akiba.

Tunazidisha mara mbili ya akiba aliyohifadhi mteja kwa wateja 100 kila mwezi. Wale watakaokaoweka akiba na sisi kipindi hiki cha kampeni watakuwa na nafasi ya kubahatika kushinda mara mbili ya Akiba yao kila mwezi. Weka kuanzia shilingi elfu kumi."

Benki hiyo imepanga kuhakikisha kuwa kampeni hiyo ni endelevu ili kuhamasisha ukuaji uchumi kwa mtu mmoja mmoja hasa wafanyabiashara wakiwamo mamalishe, waendesha bodaboda, bajaji, wamachinga na wengine.

Annastazia Yenze, kutoka Morogoro, mmoja wa washindi aliipongeza kampeni hiyo ambayo imemtia moyo katika kufanya shughuli zake za kilimo.

"Nimefurahi kushinda pikipiki hii; itanisaidia sana kama mkulima katika kusafirisha mazao yangu sokoni. Ningependa kuishukuru Benki ya NCBA kwa kampeni hii," alisema.

Washindi Salome Kapela na Ibrahim Nzunda kutoka jijini Dar es Salaam, walifurahi kupokea pikipiki hizo na kuwataka wananchi kushiriki katika kampeni hiyo.

Huduma ya Mpawa ina wateja zaidi ya milioni sita nchini kote wanaonufaika na mikopo midogo isiyokuwa na kima cha chini mpaka 500,000 wakiwa ndani au nje ya Tanzania.



Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma, Kanali Laban Thomas, akitoa maagizo kuhusu ukamilishaji wa majengo yote ya Hospitali ya Wilaya ya Namtumbo kabla ya Septemba 30, mwaka huu ili yaanze kutumika, baada ya kukagua utekelezaji wa mradi wa hospitali hiyo. **PICHA: GIDEON MWAKANOSYA**

# TCRA yatoa hadhari kwa wanaosajili laini za ndugu

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

MAMLAKA ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) Kanda ya Ziwa, imewataka watu waliotumia vitambulisho vya Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA) kusajili laini za simu za ndugu zao kujiandaa kuwajibishwa inapotokea matukio ya uhalifu wa kimtandao.

Hayo yalibainishwa jana mjini Kahama na Meneja wa TCRA, Kanda ya Ziwa, Francis Mihayo wakati wa maadhimisho ya mwaka mmoja wa redio ya Gold FM iliyopo Manispaa ya Kahama.

Sherehe hizo zilihudhuriwa na viongozi mbalimbali akiwamo Waziri wa Madini, Doto Biteko, aliyemwakilisha Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Nape Nnauye.

Alisema kila aliyesajili laini ya simu ya ndugu yake kwa kutumia namba ya kitambulisho cha NIDA ana wajibu wa kuhakikisha laini hiyo haijihusishi katika matendo ya kihalifu ikiwamo kufanya utapeli mitandaoni kwa kuwa itakapobainika watamwajibisha aliyesajili.

Mihayo alisema wanaosajiliwa namba za simu ni wenye umri chini ya miaka 18 pekee mzazi anapoona kuna ulazima wa mtoto wake kuwa na simu. Alifafanua kuwa umri zaidi ya miaka hiyo wanatakiwa kufuata sheria kwa kufanya usajili wenyewe.

"Mnaoendelea kuwasajilia laini za simu ndugu na jamaa zenu kwa kutumia namba za NIDA mlizonazo kumbukeni mna dhamana ya kuyabeba makosa yao yote pale yanapojitokeza nasi hatuwezi kuendelea kufumbia macho pale linapotokea tatizo mitandaoni na huku wahusika wanafamilia," alisema Mihayo.

Aliwataka wananchi kuingiza namba *106# kwenye simu zao kuangalia namba ya NIDA imetumika kusajili laini za simu ngapi na pale watakapoona zipo zaidi na ile anayotumia ahakikishe anatoa taarifa kwa wakala aliyemsajili na kuondolewa kabla hazijafanya uhalifu na mhusika kuwajibishwa kisheria.

Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Sophia Mjema aliipongeza Gold Fm kwa kuendelea kuelimisha jamii hususani katika chanjo mbalimbali zinazoendelea kutolewa na serikali nchi nzima ikiwamo ya UVIKO-19 pamoja na polio ya matone kwa watoto wenye umri wa chini ya miaka mitano. Kwa upande wake, Waziri wa Madini, Doto Biteko alisema, serikali imeendelea kutatua kero mbalimbali zinazoikabili sekta ya habari na sasa kumeongezeka uhuru wa kujieleza.

Alivitaka vyombo vya habari kufanyakazi kwa weledi kwa kuzingatia sheria na kanuni zilizoko ili kuepuka kupigwa faini au kufungiwa vyombo vyao.

Akizungumza katika sherehe hizo, Mkurugenzi wa Gold FM, Neema Mghen, aliomba serikali kutoa vitambulisho kwa waandishi kwa wakati (Press card) kwa kuwa kumekuwa na ukiritimba wanapoziomba.

# Hospitali ya Kisarawe yapata maji ya uhakika

**Na Joseph Mwendapole**

HOSPITALI ya Wilaya ya Kisarawe, Mkoa wa Pwani, sasa inapata maji salama na ya uhakika baada ya miundombinu kuboreshwa.

Awali, miundombinu ilikuwa chini ya Mamlaka ya Maji Kisarawe, lakini imekarabatiwa na Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA - KISARAWE), inayoisimamia kwa sasa.

DAWASA inafanya maboresho ya mfumo wa kusambaza maji kwa wateja wa taasisi kwa kuboresha miundombinu ya maji iliyorithiwa kutoka kwa Mamlaka ya Majisafi Kisarawe (KUWASA).

Akizungumza mwishoni mwa wiki, Msimamizi wa Mradi huo, Mhandisi Erasto Mwakilulele, alisema lengo la kazi hiyo ni kuwezesha upatikanaji wa huduma kwa wateja wa taasisi ambao hawana maji baada ya mfumo kushindwa kutoa huduma.

Alisema matengenezo yameanza, kazi inatarajiwa kukamilika wiki ijayo na wananchi wa maeneo hayo wanaendelea kufaidi majisafi.

Alisema, lengo la matengenezo hayo ni kusaidia kuongeza upatikanaji wa huduma kwenye maeneo yenye changamoto ya upatikanaji wa maji ikiwamo Hospitali ya Kisarawe na maeneo ya jeshi.

Aliwataja wanufaika wengine kuwa ni wakazi wa maeneo ya Mnarani zikiwamo ofisi za vyombo vya habari zilizoko kwenye eneo linalozunguka mnara pamoja na Shule ya Sekondari Minaki.

Alifafanua kuwa kazi inahusisha utoaji wa toleo la maji kutoka kwenye bomba kubwa la inchi 16 na kupeleka kwenye tangi lita 135,000 lililopo Kisarawe na kazi ya kupeleka maji kwa wateja kwa kutumia bomba la inchi nne.

Alisema kazi inatekelezwa kwa kutumia mapato ya ndani ya mkoa wa kihuduma Kisarawe.

"Tumeona kuna kila sababu ya wateja wa taasisi kupata huduma na hivyo tumeamua kufanya maboresho haya ili huduma iweze kupatikana muda wote," alisema Mhandisi Erasto.

Aliongeza kuwa baada ya kukamilika kwa matengenezo hayo, huduma itapatikana kwa ubora zaidi kwa wateja waliotajwa.

Wakati huo huo (DAWASA), imesema inaendelea kufanya maboresho makubwa ya miundombinu ya majisafi eneo la Tabata Kisiwani ili kuhakikisha huduma inamfikia kila mwananchi.

Imesema eneo la Tabata Kisiwani lina changamoto ya kuvuja kwa maji mara kwa mara kutokana na ubovu wa miundombinu na kupitia maboresho hayo imepata ufumbuzi wa kudumu.

Meneja wa DAWASA Tabata, Mhandisi Boniphace Ole, alisema kazi ya maboresho imeshaanza na inatekelezwa usiku na mchana na kukamilika kwake kutamaliza changamoto ya upotevu wa maji eneo la Tabata Kisiwani.

"Tumeamua kufanya maboresho haya kutokana na eneo hilo kuwa korofi kwa changamoto ya kuvuja maji mara kwa mara, lengo letu ni wananchi wa Tabata Kisiwani wapate huduma bora ya majisafi muda wote," alisema Mhandisi Ole.

# Mwenyekiti wa UVCCM ataka umoja, mshikamano

**Na Saada Akida**

MWENYEKITI wa Umoja wa Vijana CCM (UVCCM) Wilaya la Mkuranga, Abdallah Ngwenda, amewataka viongozi wa serikali za mitaa, kata na madiwani kujiweka kando na masuala ya siasa na itikadi ya vyama katika maendeleo wilayani humo.

Alitoa rai hiyo juzi wakati wa kongamano lililoandaliwa na jukwaa la vijana kwa ajili ya utekelezaji wa mradi wa elimu, uzalendo na maadili kwa vijana katika Kijiji cha Mwandege mkoani Pwani.

Akizungumza na Nipashe, Ngwenda alisema masuala ya maendeleo ya vijana, viongozi wa ngazi za chini wanatakiwa kuwasaidia vijana bila kujali itikadi za vyama vyao.

Aliwataka viongozi hao kuweka pembeni masuala ya siasa kwa ajili ya kumuunga mkono Rais Samia Suluhu Hassan anayetaka kuona vijana wanapata maendeleo na kusonga mbele kimaisha.

"Viongozi mlichukuwa dhamana la kusaidia serikali huku chini tunawaamini mnatakiwa kutoa taarifa na kuunga mkono juhudi za vijana katika masuala haya ya makongamano yanayowasaidia kuleta maendeleo ya Taifa," alisema Ngwenda na kuongeza:

"Kila maeneo tukipeleka siasa hatuwezi kufikia juhudi za Rais Samia Suluhu Hassan, tunatakiwa kuweka makandokando yetu pembeni na kubeba dhamana ya uongozi tuliyopewa na kuaminiwa na hawa vijana ili tulete maendeleo."

Alisema ana imani vijana ni nguzo muhimu katika maeneo yao ikiwamo masuala ya kisiasa.

"Mara nyingi viongozi tunapata nafasi ya kukutana na mkuu wa wilaya na kujadili maendeleo, sio kila muda kuzungumza mambo ya siasa na kuacha uhalisia," alisema.

Mwenyekiti wa Jukwaa la Vijana Kata ya Mwandege, Laurent Fabian, alisema malengo makubwa waliyonayo ni kuwajenga uwezo vijana wawe wazalendo na kupenda nchi yao ili kuwa walinzi wa amani ya kijiji, wilaya na taifa.

"Jukwaa letu linaunganisha vijana kujadili matatizo yanayotukabili na kuwasilisha serikalini baada ya kukaa vijiweni na kuishia kulalamika, jukwaa hili tunatoa elimu ya afya ya uzazi, stadi za maisha na usajiriamali na kuanzisha vikundi mbalimbali kwa vijana waliopo vijiweni kuweza kujishughulisha."

Alisema wako kwenye mchakato wa kuanzisha mfuko kwa ajili ya kusaidia vijana wa Kijiji cha Mwandege kusonga mbele katika maendeleo na kuachana na kukaa vijiweni kwa sababu ni wakati wa kutazama maendeleo ya taifa.

# Mabaraza ya kata yapigwa 'stop' utatuzi migogoro ardhi

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

SERIKALI imefanya marekebisho ya Sheria ya Mahakama ya Utatuzi wa Migogoro ya Ardhi namba 216 kwa mabaraza ya kata kuondolewa uwezo wa kusikiliza mashauri ya ardhi kama yalivyokuwa yakifanya awali.

Mwenyekiti wa Baraza la Ardhi Wilaya ya Singida, Bahati Colex, alisema hayo juzi wakati wa semina ya wenyeviti wa mabaraza ya kata wa Manispaa ya Singida.

Alisema marekebisho hayo yanalenga kuboresha utoaji haki hasa ikizingatiwa kuwa jukumu hilo lilipewa mabaraza ya kata ambayo kimsingi wajumbe wake sio wataalamu wa sheria.

Colex alisema kutokana na marekebisho hayo ya sheria ambayo yalianza kutumika Oktoba 11, mwaka jana, mabaraza ya kata yamepewa jukumu la usuluhishi.

Alisema endapo usuluhishi ukishindikana mabaraza ya kata yatatoa cheti cha usuluhishi ili wadaawa waweze kufungua shauri kwenye baraza la ardhi na nyumba wilaya.

"Kifungu cha 45 cha sheria hii kimerekebisha kifungu cha 13 (2) na kuyapa mabaraza ya kata jukumu la usuluhishi tu badala ya kusikiliza kesi na kutoa hukumu, sasa mabaraza ya kata yanapaswa kusuluhisha mgogoro wa ardhi kati ya wadaawa (mlalamikaji na mlalamikiwa) ndani ya siku 30 kwa mujibu wa Kifungu cha 13 (4)," alisema.

Colex alisema kwa mujibu wa mabadiliko hayo mashauri yote ya ardhi yataanzia kwenye mabaraza ya kata bila kujali thamani ya ardhi husika.

Alisema baraza la kata likishindwa kuwasuluhisha wadaawa, litatoa cheti au hati ya usuluhishi na watakuwa na nafasi ya kufungua shauri lao la ardhi katika baraza la ardhi na nyumba wilaya.

Alisema endapo siku 30 zitapita tangu lalamiko lilipopelekwa baraza la kata bila kusuluhishwa, mlalamikaji anaruhusiwa kufungua shauri lake mbele ya baraza la ardhi na nyumba wilaya bila hata kuwa na cheti cha usuluhishi.

Aliongeza kuwa sheria hiyo pia inampa mamlaka Waziri wa Sheria akishirikiana na Waziri wa Ardhi kutengeneza kanuni zitakazosimamia uendeshaji wa usuluhishi mbele ya mabaraza ya kata.

Colex alisema kuhusu mashauri ya ardhi yaliyofunguliwa kabla ya Oktoba 11, mwaka jana mbele ya mabaraza yataendelea kwa utaratibu wa zamani na yatatolewa hukumu.

Mwanasheria wa Manispaa ya Singida, Burton Mahenge, alisema wajumbe wa baraza la kata wanapomaliza muda wao wa miaka mitatu wawe wanatoa taarifa mapema ili kutoa fursa kufanyika mchakato wa kupata wajumbe wapya.

Mahenge alisema wajumbe wanapochelewa kutoa tangazo la kumaliza muda wao kunasababisha uchelewaji wa usikilizwaji wa mashauri.




Mkuu wa Idara ya Sheria na Katibu wa Benki ya KCB Tanzania, Antonia Kilama, akipokea cheti cha kuhitimu mafunzo maalumu ya uongozi kutoka kwa Naibu Katibu Mkuu, Wizara ya Fedha na Mipango-Sera, Lawrence Mafuru, katika mahafali ya pili ya Umoja wa Maofisa Watendaji Wakuu wa Kampuni Binafsi nchini (CEOrt). Kushoto ni Mwenyekiti wa CEOrt, David Tarimo. Mafunzo hayo ni mahusisi kwa ajili ya kuwaandaa viongozi kwa ajili ya kushika nafasi za juu kwenye taasisi hapa nchini. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Waandishi wafundwa kuzingatia usawa kijinsia

**Na Sabato Kasika**

WAANDISHI wa habari wametakiwa kutumia kalamu zao kuhamasisha jamii kutambua umuhimu wa usawa wa kijinsia ili kuwapo na uwiano kati ya wanaume na wanawake katika ngazi mbalimbali za uamuzi.

Wito huo ulitolewa na Mkurugenzi Mtendaji wa taasisi isiyo la kiserikali inayojishughulia kubadili maisha ya wanawake, vijana na watoto (TIBA), Marcela Lungu, katika mafunzo ya kuwajengea uwezo wa kitaaluma waandishi wa habari kuhusu masuala la jinsia.

"Uongozi katika jicho la jinsia ni dhana pana inayolenga kuongeza ushiriki wa wanawake ili kuwa na uwiano wa sauti au uwakilishi unaolingana katika siasa na ngazi za kufanya maamuzi," alisema Marcela.

Pia, kutokana na upana wa dhana hiyo, waandishi hawana budi kujua kuwa uongozi unawakilisha makundi mbalimbali na wanatakiwa kuhamasisha kuwapo kwa uwiano ili kuwa na uwakilishi mpana.

"Jinsia maana yake ni mgawanyo wa majukumu, hivyo toeni mchango wa kuhamasisha usawa wa kijinsia ili kusaidia juhudi zinazofanywa na Rais Samia Suluhu Hassan za kuendelea kutafuta asilimia 50 kwa 50," alisema.

Mtaalamu wa masuala ya habari wa Taasisi ya Internews ilioandaa mafunzo hayo, Alakok Mayombo, alisema, waandishi watakiwa kuandika habari zinazoleta mabadiliko katika jamii.

"Kupitia kalamu, waandishi wanaweza kubadilisha mfumo na kuwapo waandishi wanawake ambao ni wa kutolea mfano katika kazi zao, kushiriki kuandaa stori zinazozalisha viongozi wengi wanawake," alisema Alakok.

Alifafanua kuwa kuandika stori zinazohusu wanawake kupigwa au kubakwa sio vibaya, ila zinaelekeza mamlaka kuchukua hatua na kwamba ni muhimu kuhamasisha wanawake kupanda juu wengine kufuata nyayo hizo.

Ofisa Mradi Mwandamizi wa Internews, Victoria Rowan, alisema ni muhimu waandishi kuelimisha umma kuwa suala la kutafuta usawa wa kijinsia, halihusu wanawake pekee bali na wanaume.

"Usawa wa kijinsia ni muhimu kwa pande zote mbili kwa kutambua kuwa suala la uongozi linahusu akili na uwezo wa kuongoza, halibagui jinsi, hivyo ni muhimu waandishi kulitambua hilo," alisema Victoria.

Alisema kumekuwapo na kutojua usawa wa kijinsia na kwamba taasisi inaweza ikamuomba mhariri kutuma mwandishi kushiriki mafunzo ya usawa huo na kujibiwa kuwa hayo yanahusu waandishi wa kike.

Mhadhiri Msaidizi wa Shule Kuu ya Uandishi wa Habari ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (SJMC), Zuhura Seleman, alisema kuna mtazamo hasi kuwa wanaume wana akili kuliko wanawake.

Alisema waandishi pia wanatakiwa kuwa jicho la usawa wa kijinsia na kwamba kwa kila habari wanazoandika ziwe zinazingatia mambo ya sera, bajeti na afya ili kubaini kama kuna usawa huo.

Mkuu wa Miradi Shirika lisilo la kiserikali la C-SEMA, Michael Marwa, alisema vyombo vya habari vina uwezo wa kuchochea usawa wa kijinsia katika jamii na kubadili mtazamo hasi wa jamii.

Nipashe
Spotika



VIUNGO WASHAMBULIAJI 5-BORA ZAIDI KWA SASA UK. 12-13



# KLABU 5 ZILIZOMKATAA RONALDO MSIMU HUU

## ISIKUPITE

CRISTIANO Ronaldo ndiye mchezaji anayecheza soka hadi sasa ambaye amefunga mabao mengi kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya, akiwa amecheka na nyavu mara 140 katika mechi 183, akifuatiwa na Lionel Messi (mabao 125, mechi 156), Robert Lewandowski (mabao 86, mechi 106), Karim Benzema (mechi 86, mabao 142) na Thomas Muller (mabao 52, mechi 134).



**MANCHESTER,** England

CRISTIANO Ronaldo alikuwa akitafuta namna ya kuondoka Manchester United majira yote haya ya joto, lakini juhudi zake zimegonga mwamba. Nyota huyo wa Ureno alichukizwa na hali ambayo hakuridhika nayo pale United katika hatua za mwanzo za dirisha la usajili la majira ya joto na akataka kuondoka.

Man United walimaliza vibaya msimu wa 2021-22 na walishindwa kufuzu Ligi ya Mabingwa Ulaya baada ya kumaliza nafasi ya sita kwenye msimamo wa Ligi Kuu. Ronaldo alitwaa tuzo ya 'Sir Matt Busby' ya Mchezaji Bora wa Mwaka' katika klabu ya Man United msimu uliopita.

Hata hivyo, kutokana na umri wake, timu hazijawa tayari kumchukua mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 37. Hebu sasa tuangalie klabu tano ambazo zimemkataa nyota huyo msimu huu wa majira ya joto...

### #5. BORUSSIA DORTMUND

Borussia Dortmund ni moja ya klabu ya karibuni sana kumkataa Ronaldo. Kwa mujibu wa Jarida la Ujerumani la Bild (kupitia The Mirror), mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 37, alikuwa ameweka macho yake kwenye kikosi hicho cha Bundesliga kama mahali pazuri pa kufika, lakini Dortmund hawakuonyesha kumhitaji.

Inadaiwa wakala wa Ronaldo, Jorge Mendes, alimtoa kwa Dortmund lakini walikataa wazo hilo. Dortmund hawakuwa na nia ya kumlipa mshindi huyo mara tano wa tuzo ya Ballon d'Or mshahara mkubwa.

Ukweli ni kwamba waliamua kutomsajili licha ya kutokuwapo kwa nyota wao, Sebastian Haller ambaye aligundulika kuwa na uvimbe wa tezi dume.

Katika mkutano na waandishi wa habari Ijumaa ya (Agosti 19), Mkurugenzi Mtendaji wa Dortmund, Hans-Joachim Watzke alitupilia mbali wazo la nyota huyo wa zamani wa Real Madrid kuwasili hapo Signal Iduna Park. Alisema (kupitia ProSoccerWire):

"Ninampenda mchezaji huyu, hakika ni wazo la kupendeza kuona Cristiano Ronaldo akicheza kwenye Uwanja wa Signal Iduna Park. Lakini hakuna mawasiliano yoyote yaliyofanyika. Kwa hiyo unapaswa kuacha kuzungumza juu yake."

### #4. ATLETICO MADRID

Inashangaza kwamba Ronaldo aliripotiwa kutolewa kwa Atletico Madrid na Jorge Mendes mapema msimu huu wa majira ya joto. Hata hivyo, kwa mujibu wa ripoti ya Marca (kupitia Times Now), 'Rojiblancos' hao ambao ni wapinzani wa jiji moja na klabu ya zamani ya mchezaji huyo, Real Madrid, hawakuwa tayari kuunga mkono wazo hilo kutokana na sababu za kiuchumi.

Rais wa Atletico Madrid, Enrique Cerezo pia alitupilia mbali wazo la nyota huyo kutua Madrid. Akikiambia kipindi cha Redio El Partidazo de COPE:

"Sijui ni nani aliyevumbua hadithi hii kuhusu Cristiano Ronaldo kwenda Atletico Madrid. Hakika si kweli. Kwa kweli haiwezekani kwake kuja Atletico Madrid."

Muda mfupi baada ya tetesi zinazomhusisha na Atletico kuibuka, mashabiki wakuu wa klabu hiyo walijitokeza na bango kubwa lenye ujumbe ' Ronaldo hakaribishwi', wakati wa mechi yao ya kirafiki ya kujiandaa na msimu mpya dhidi ya Numancia mwishoni mwa Julai.

### #3. PARIS SAINT-GERMAIN

Mashabiki wangependa kuona Ronaldo akishirikiana na Lionel Messi angalau mara moja katika maisha yao ya soka. Lakini wazo hilo linaweza kubaki kuwa ndoto ingawa Paris Saint-Germain ilidaiwa kufanya mazungumzo na wakala wake Mendes.

Lakini mabingwa hao wa Ligue 1 hawakuwa na nia ya kumsajili kwani hawakumwona kama kitu kinachohitajika. PSG tayari ina Lionel Messi, Kylian Mbappe, na Neymar kwenye kikosi chao.

Wachezaji hawa wote watatu wanalipwa kiasi kikubwa cha mishahara na PSG hawakuwa na nia ya kutimiza matakwa ya mshahara wa fowadi huyo.

### #2. BAYERN MUNICH

Bayern Munich ilikataa waziwazi wazo la kumsajili Ronaldo msimu huu wa majira ya joto. Mendes alikuwa tayari kumtoa nyota huyo kwa 'Bavaria' hao na walitafakari hatua hiyo kabla ya kuamua kutoifuatilia. Oliver Kahn, rais wa Bodi ya Wakurugenzi ya Bayern Munich, aliiambia Kicker (kupitia Marca):

"Tulijadiliana kuhusu Cristiano Ronaldo ndani - ninamwona kuwa mmoja wa wanasoka bora kabisa. Kisha tukafikia hitimisho kwamba, licha ya kuthaminiwa kwa Cristiano, hatafaa katika falsafa yetu katika hali ya sasa."

### #1. CHELSEA

Kwa mujibu wa The Athletic, Ronaldo alikuwa analengwa na Chelsea msimu huu wa majira ya joto. Mmiliki mpya wa Chelsea, Ted Boehly, inasemekana alikutana na Mendes kujadili uwezekano wa uhamisho wa fowadi huyo maarufu wa Ureno katika hatua za mwanzo za dirisha la uhamisho. Lakini baada ya mazungumzo na kocha Thomas Tuchel, 'The Blues' waliamua kuachana na mpango wa kumsajili.

Uamuzi huo uliripotiwa kuwa Tuchel aliona si jambo muhimu kwa sasa kumleta Ronaldo pale Stamford Bridge.

## Extra Time

# VIUNGO WASHAMBULIAJI 5-BORA ZAIDI KWA SASA




**LONDON,** England

KIUNGO mshambuliaji au namba 10 ndiye mbunifu mkuu wa timu. Anakaa nyuma ya washambuliaji na ana jukumu la kuwatengenezea nafasi. Washambuliaji wa kati wanaweza kuwa nyenzo ya kweli kwa mawazo yao ya haraka na utekelezaji.

Baadhi ya wachezaji wanaoheshimika zaidi katika historia ya soka ni washambuliaji wa kati. Diego Maradona, Zinedine Zidane, Johan Cruyff, Kaka, Michel Platini na Zico ni baadhi ya viungo washambuliaji wanaotambulika zaidi katika historia ya soka duniani.

Kuna viungo wengi wa ushambuliaji wa kiwango cha kimataifa duniani hivi sasa. Ingawa majukumu yao yanafanana zaidi au kidogo, wasifu wao unaweza kutofautiana. Baadhi ni bora katika kucheza pasi ambazo wengine wanaweza hata wasifikirie, wakati wengine wanaweza kuvinjari nafasi zilizobana vizuri zaidi kuliko zingine.

Ngoja tuwatazame viungo washambuliaji watano bora zaidi duniani kwa sasa, twende...

### #5. HAKAN CALHANOGLU (INTER MILAN)

Hakan Calhanoglu aliondoka AC Milan na kujiunga na Inter Milan msimu wa majira ya joto wa 2021, kiasi cha kuzomewa na mashabiki wa 'Rossoneri' hao. Haikumchukua muda mrefu sana kuwa sehemu muhimu ya 'Nerazzurri' na uwezo wake wa kushawishi kucheza katika tatu ya mwisho.

Kiungo huyo wa kati wa kimataifa wa Uturuki, alikuwa tayari amejidhihirisha kuwa mmoja wa washambuliaji bora kwenye Ligi Kuu ya Italia, Serie A, wakati akiwa na AC Milan. Katika msimu wa 2021-22, aliunda safu ya ushambuliaji ya kutisha huku Edin Dzeko na Lautaro Martinez wakiwa juu pale Inter Milan.

Michango ya Calhanoglu na Nicolo Barella katika safu ya kiungo, ilikuwa muhimu kwa Inter kutwaa ubingwa wa Serie A msimu uliopita. Bahati mbaya kwa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 28, klabu yake ya zamani ya AC Milan ilikipiku kikosi hicho cha Simone Inzaghi na kutwaa ubingwa msimu uliopita.

Katika mechi 46 kwenye michuano yote msimu uliopita, Calhanoglu alifunga mabao nane na kutoa pasi 13 za mabao.

### #4. MARCO REUS (BORUSSIA DORTMUND)

Marco Reus amekuwa bora kwenye namba 10 ya Borussia Dortmund katika misimu ya hivi karibuni. Akiwa na umri wa miaka 33, Reus amekuwa mtu wa klabu moja.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Ujerumani, ni mmojawapo wa vipaji bora zaidi vya kizazi chake na angeweza kupata umaarufu kwa urahisi kama kazi yake isingeathiriwa na majeruhi. Reus daima amekuwa mtu wa kutisha ndani na karibu na tatu ya mwisho.

Yeye ni bora akiwa na mpira miguuni mwake na miguso yake ya ustadi na kasi. Pia ni mmaliziaji mzuri na huonyesha utulivu mwingi anapopewa nafasi za kufunga mabao.

Katika msimu wa 2021-22, Reus alifunga mabao 13 na kutoa asisti 19 katika mechi 41 kwenye mashindano yote akiwa na Borussia Dortmund.

### #3. MASON MOUNT (CHELSEA)

Si kila siku kipaji kutoka akademi ya Chelsea kinaweza kufanya makubwa kwa klabu. Kwa bahati nzuri kwa Mount, alifanikiwa katika kipindi chake cha mkopo akiwa Derby County chini ya ulezi wa Frank Lampard, ambaye baadaye akawa kocha wa Chelsea msimu uliofuata.

Mount anauwezo wa kucheza popote kwenye mstari wa mbele, lakini anakuwa kwenye kiwango bora zaidi anapocheza nyuma ya washambuliaji wawili. Katika misimu michache iliyopita, Mount amekuwa mmoja wa viungo washambuliaji bora kwenye Ligi Kuu England.

Anajua kuchezea vizuri ndani ya tatu ya mwisho na ana uwezo wa kuona mikimbio ya wachezaji wenzake. Mount ni mmoja wa wachezaji muhimu wa Chelsea na timu ya Taifa ya England hivi sasa.

Katika mechi 53 kwenye michuano yote aliyoichezea Chelsea msimu wa 2021-22, alifunga mabao 13 na kutoa asisti 16.

### #2. THOMAS MULLER (BAYERN MUNICH)

Anayejiita 'Raumdeuter' au 'mkalimani wa nafasi', Thomas Muller, ni mwanasoka wa ajabu. Ni mmoja wa wanasoka mahiri na wenye akili sana kwa kizazi chake na ni ndoto ya mshambuliaji yeyote kucheza naye.

Uchezaji wa kiungo wa Muller na harakati zake ni za kiwango cha kimataifa na pia hucheza soka ya kiwango cha juu. Na katika kazi yake yote, ameonyesha uwezo wa kudumisha utulivu wake katika hali ngumu. Hilo ndilo limemfanya kuwa 'mfalme wa asisti' wa Ulaya.

Aliunda safu bora zaidi ya wawili alipokuwa na Robert Lewandowski pale Bayern Munich. Katika mechi 45 katika michuano yote aliyoichezea Bayern msimu wa 2021-22, Muller alifunga mabao 13 na kutoa asisti 25.

### #1. KEVIN DE BRUYNE (MANCHESTER CITY)

Kevin De Bruyne alichaguliwa kuwa Mchezaji Bora wa Msimu wa Ligi Kuu England msimu uliopita. Kiungo huyo wa kati wa Manchester City ndiye kiungo mshambuliaji bora zaidi wa kizazi chake. Ana uwezo mkubwa wa kutoa pasi yenye macho.

De Bruyne amekuwa mchezaji mkuu wa Man City enzi za Pep Guardiola. Ushujaa wake umeifanya City kunyakua mataji manne ya Ligi Kuu katika misimu mitano iliyopita, mataji matano ya Ligi na Kombe la FA moja. Mchezaji huyo wa kimataifa wa Ubelgiji ni mmoja kati ya viungo bora zaidi wa kizazi chake duniani.

Ana uwezo wa kuwachezesha wachezaji wenzake popote pale uwanjani kwa usahihi. Katika mechi 45 kwenye mashindano yote msimu wa 2021-22, mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 31, alifunga mabao 19 na kutoa asisti 14.

## Nukuu

"Wako katika ulimwengu tofauti, wana ubora tofauti. Unapocheza dhidi ya Messi [Lionel], hisia unazokuwa nazo ni juu yake tu, ikiwa yuko katika hali nzuri au ana siku njema, huwezi kumzuia. Hayo ni maoni yangu ya ukweli. Hali hiyo hiyo inatumika kwa Ronaldo [Cristiano]. Wana njia mbili tofauti za kucheza, moja ya kujaribu na kufunga mabao na nyingine ni kufurahia soka lake. Kama nikichagua mmoja, itakuwa Messi. Je, yeye ndiye bora zaidi kuwahi kutokea? Sikumwona Pele au Diego Maradona wakicheza kwa sababu huo haukuwa wakati wangu, hivyo ni Messi,"
**Beki wa Real Madrid, Antonio Rudiger kuhusu nani bora kwake kati ya Messi na Ronaldo**




"Kusema ukweli, nadhani ili kuchambua timu ninayoikubali, lazima uangalie mechi za kufuzu [Kombe la Dunia] zilivyokuwa. Na leo, Argentina na Brazil wanapewa nafasi zaidi juu ya timu za Ulaya,"
**Mshambuliaji na Kocha wa zamani wa Ujerumani, Jurgen Klinsmann kuelekea Kombe la Dunia nchini Qatar 2022.**



"Naunga mkono mambo mengi ya VAR, kwa kweli nadhani kipa anajirusha, anadanganya kuwa ameumia kwa sababu hawezi kumfika mwingine. Alifanya vivyo hivyo kwenye goli la kwanza pia. Mwamuzi kwa namna fulani anakosea ni ajabu,"
**Kocha wa West Ham United, David Moyes akimtuhumu Kipa wa Chelsea, Edouard Mendy, kwa kujiangusha na kudanganya kuwa ameumia wakati 'The Blues' ikishinda 2-1.**





Wachezaji wa Nyasa Big Bullets wakishangilia moja ya mabao yao kwenye Ligi Kuu nchini Malawi. **PICHA: MTANDAO**

# USIYOYAJUA WAPINZANI WA SIMBA, YANGA CAF

**Na Adam Fungamwango**

HII ni wiki ambayo klabu tano za Tanzania zinakwenda kuanza rasmi safari ya mechi za kimataifa, Ligi ya Mabingwa Afrika na Kombe la Shirikisho.

Kuanzia Jumamosi ijayo Simba, Yanga, KMKM, Geita Gold na Kipanga zitakuwa vitani zikisaka ushindi kwenye mechi zao ili kujiweka kwenye mazingira mazuri kabla ya mechi za marudiano. Ni Azam FC pekee ambayo haitocheza wiki hii kwa sababu yenyewe itaanzia raundi ya kwanza, huku mechi zitakazochezwa wiki zikiwa ni raundi ya awali.

Mabingwa Watetezi wa Ligi Kuu Bara, Yanga watakuwa uwanjani kucheza dhidi ya Zalan FC ya Sudan Kusini, Simba ikienda ugenini nchini Malawi kucheza dhidi ya Nyasa Big Bullets, KMKM itaanzia nyumbani dhidi ya Al Ahli Tripoli ya Libya. Hizi zote ni mechi za Ligi ya Mabingwa Afrika.

Kwenye Kombe la Shirikisho barani Afrika, Geita Gold itaanzia ugenini dhidi ya Hilal Alsahil ya Sudan, huku Kipanga nayo ikianza ugenini Sudan Kusini dhidi ya Al Hilal Wau.

Katika makala haya tutazichambua timu ambazo zitacheza na wawakilishi wa Tanzania kwenye michuano ya kimataifa kuanzia Septemba 10, twende sasa...

### NYASA BIG BULLETS (MALAWI)

Timu hii ilianzishwa mwaka 1967 ikiitwa Nyasaland, lakini baadaye ikaanza kudhaminiwa na Kampuni ya Viatu ya Bata, ikaanza kuitwa Bata Bullets.

Ilikuwa ni moja kati ya timu tishio kwenye Ukanda wa Afrika Mashariki na Kati hususan katika michuano ya kombe hilo ambalo kwa sasa linaitwa Kombe la Kagame. Maskani ya klabu hiyo ni Blantyle na kwa sasa inadhaminiwa na Nyasa Manufacturing Company (NMC).

Mabingwa hao wa sasa wa Malawi, watacheza nyumbani kwao dhidi ya Simba Jumamosi wiki hii na marudiano yatakuwa kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Septemba 18.

Wakati ligi ya Malawi inaendelea, timu hiyo ipo kileleni ikiwa na pointi 52 mpaka sasa, ikicheza mechi 20, ikishinda 16, imetoka sare nne ikiwa haijapoteza mechi yoyote ile.

Mbali na hayo inaonekana ina mastraika wazuri kwani imepachika mabao 46 mpaka sasa na kufungwa 11 tu.

### ZALAN FC (SUDAN KUSINI)

Ni timu ngeni kwenye masikio ya mashabiki wengi wa soka Afrika. Itaanzia raundi ya awali dhidi ya Mabingwa wa Tanzania, Yanga.

Itacheza mechi yake ya kwanza ikiwa nyumbani kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, yenyewe ikiomba hivyo kutokana na hali ya usalama nchini kwao Sudan ya Kusini. Maskani yake ni maeneo ya Rambek. Itachezwa Jumamosi wiki hii na mechi ya marudiano itachezwa siku saba baadaye kwenye uwanja huo huo.

Ilichukua ubingwa nchini humo msimu uliomalizika uliowawezesha kucheza Ligi ya Mabingwa, pia iliwahi kutwaa Kombe la Shirikisho la Soka Sudan mwaka 2018/19. Mpaka sasa ligi ya Sudan Kusini msimu huu bado haijaanza.

### AL AHLLI TRIPOLI (LIBYA)

Ni moja kati ya timu kubwa nchini Libya inayokuja kwa kasi kwenye michuano ya kimataifa hivi sasa. Ikumbukwe kuwa msimu uliomalizika ilitolewa kwenye hatua ya robo fainali na wapinzani wa jadi nchini kwao, Al Ittihad kwa bao 1-0, zikitoka suluhu kwenye mechi ya kwanza na marudiano ilichapwa bao 1-0 na kuondolewa kwenye hatua hiyo.

Haitakuwa mara ya kwanza kuja nchini, kwani ilishawahi kufika mwaka 2021 ikacheza dhidi ya Biashara United Oktoba 15 na kufungwa mabao 2-0, lakini wawakilishi wa Tanzania walishindwa kwenda Libya na kung'oka kwenye michuano hiyo ya Shirikisho.

Msimu huu inacheza Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya wawakilishi wa Tanzania Visiwani, KMKM. KMKM itaanzia nyumbani Jumamosi wiki hii, kabla ya kwenda jijini Tripoli kucheza mechi ya marudiano Septemba 17 kwenye hatua za awali za michuano hiyo. Mpaka sasa Ligi ya Libya kwa msimu huu haijaanza.

### HILAL ALSAHIL (SUDAN)

Ni timu kutoka Sudan ambayo msimu uliopita ilishika nafasi ya tatu, ikipata nafasi ya kuiwakilisha nchi hiyo kwenye michuano ya Kombe la Shirikisho Afrika.

Timu hiyo ambayo inatoka maeneo ya Port Sudan, itacheza dhidi ya Geita Gold Jumapili wiki hii, ikianzia nyumbani nchini Sudan, na Septemba 17 zitarudiana nchini Tanzania.

Geita Gold ni mara yake ya kwanza kushiriki mchuano ya kimataifa, lakini kutokuanza kwa ligi ya Sudan, huku yenyewe ikiwa imecheza angalau mechi tatu za Ligi Kuu Tanzania Bara, inaweza kuwa faida kwao.

### AL HILAL WAU (SUDAN KUSINI)

Itacheza na Kipanga ya Zanzibar kwenye michuano ya Kombe la Shirikisho. Timu hiyo inayotoka Sudan ya Kusini na si maarufu sana kwenye soka la kiafrika.

Itaanzia nyumbani Jumapili hii na kurudiana tena Septemba 17 mjini Zanzibar kwenye hatua hiyo ya awali ya michuano hiyo.

## JE, WAJUA?

HADI kufikia mzunguko wa pili wa mechi za Ligi Kuu Bara, Klabu ya Simba mbali ya kuwa kileleni mwa msimamo wa ligi hiyo, ndiyo inayoongoza kwa kupiga pasi nyingi, ikiwa na pasi 847, ikifuatiwa na Azam FC (pasi 797), Yanga (pasi 736), Ihefu FC (pasi 524) na Namungo (pasi 511).





## Serikali kuhakikisha makundi yote yananufaika na fursa

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SERIKALI imedhamiria kuhakikisha makundi yote katika jamii yanashiriki kikamilifu kwenye utekelezaji wa mipango, sera na miongozo inayoandaliwa ili kila mmoja anufaike na fursa zilizoko.

Kaimu Katibu Mkuu, Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Amon Mpanju, alisema hayo alipokuwa akifungua kikao cha wadau wanaopitia na kutoa maoni juu ya kitini cha mwongozo kuhusu mafunzo ya uwiano wa kijinsia na ushirikishwaji wa jamii, kinachofanyika jijini hapo.

Mpanju alisema mwongozo utatumika kuhakikisha kwenye huduma zote zinazotolewa nchini zinazingatia uwiano na usawa wa kijinsia na ujumuishaji wa jamii.

"Kwa kawaida unapotaka kuongelea maendeleo na ustawi lazima uyape mahitaji yake jicho la kipekee ili Maofisa Ustawi na Maofisa Maendeleo ya Jamii wanapotoa huduma kwa jamii wazingatie upekee kwa makundi hayo," alisema.

Alimwagiza Kamishna wa Ustawi wa Jamii kuhakikisha mwongozo huo unasambazwa kwa wadau wote ili makundi yote maalum yajumuishwe kwenye mnyororo mzima wa maendeleo na ustawi wa jamii.

Awali, akitoa maelezo ya mwongozo huo, Mtaalamu Mshauri wa Masuala ya Jinsia kutoka Shirika la PACT, Beatrice Sandegea, alisema lengo ni kuhakikisha wataalamu wa ustawi wa jamii na watoa huduma ngazi ya jamii wote wanatambua matatizo ya kijinsia wakati wa ushirikishwaji wa shughuli mbalimbali za kijamii na kuyatafutia ufumbuzi.

"Mwongozo huu utaelezea pia namna ya kuingiza uwiano wa kijinsia ndani ya sera, mipango na miongozo ya kitaifa ya huduma za ustawi wa jamii na katika programu za kazi zote, tunapotoa huduma za ustawi kwa kuzingatia makundi yote," alisema.

Alibainisha rasimu ya mwongozo huo ulifanyiwa majaribio kwa watoa huduma 110 katika mikoa sita na kuonesha ufanisi kwenye kutambua matatizo na kutafuta namna ya kutatua kwa kutumia rasilimali walizonazo.

"Ndani ya jamii ndipo wanapoanza kuwaficha makundi mengine kwa mfano watoto wenye ulemavu hivyo mwongozo unalenga kuhakikisha wanapotoa huduma hakuna mtu anayeachwa," alisema.

Kwa upande wake, Kamishna wa Ustawi wa Jamii, Dk. Nandera Muhando, alisema mchakato wa kuandaa mwongozo huo ulianza tangu mwezi Juni mwaka huu kutokana na utafiti mbalimbali kuonesha kuna tatizo la ushirikishwaji wa makundi yenye mahitaji maalum.



Makamu Mwenyekiti Kamati ya Kudumu ya Bunge Hesabu za Serikali za Mitaa (LAAC), Selemani Zedi, akiongoza kikao cha kamati hiyo mwisho wa wiki Bungeni jijini Dodoma. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# PAC yaiagiza OSHA kuelimisha wananchi usalama afya kazini

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

KAMATI ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC) imeutaka Wakala wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi (OSHA) kuongeza uelewa wa masuala ya usalama na afya kwa Watanzania ili kupunguza ajali, magonjwa na vifo vinavyotokea maeneo ya kazi.

Mwenyekiti wa PAC, Naghenjwa Kaboyoka, alitoa agizo hilo juzi baada ya kuhitimishwa kwa mafunzo ya usalama na afya pamoja na upimaji afya lililoandaliwa na OSHA kwa kamati hiyo.

"Wajumbe wangu kwa kweli wamefurahi sana maana wamejua mambo mengi sana kupitia mada nzuri zilizowasilishwa na wataalamu wa OSHA. Tathmini ambayo tunatoka nayo baada ya mafunzo haya ni kwamba OSHA inafanya kazi nzuri, lakini tunawashauri kujitangaza na kutoa elimu zaidi kwa wananchi ili kuwasaidia waajiri na wafanyakazi kujua wajibu wao kuhusiana na usalama na afya mahali pa kazi," alisema Kaboyoka.

Pia alisema kamati imeridhishwa na ujenzi wa jengo jipya la OSHA kwa kuzingatia viwango stahiki kulingana na thamani ya fedha.

Mbunge wa Ngorongoro, Emmanuel Shangai, alisema: "Nimeona thamani halisi ya fedha katika jengo, limejengwa vizuri na limezingatia mahitaji ya watu wenye ulemavu na taratibu zote za usalama na afya. Tunatoa wito kwa taasisi nyingine kuiga mfano huu."

Awali, Mtendaji Mkuu wa OSHA, Khadija Mwenda, aliieleza kamati hiyo masuala mbalimbali ikiwamo namna ilivyotekeleza mradi huo wa jengo la ofisi la ghorofa nne kwa miezi minane na kutumia kiasi cha Sh. bilioni 4.8 chini ya bajeti ya Sh. bilioni 6.5 pamoja na kodi.

Naye Mwenyekiti wa Bodi ya OSHA, Dk. Adelhelm Meru, aliahidi kutekeleza ushauri uliotolewa na kamati hiyo yenye wajibu wa kusimamia nidhamu katika matumizi ya fedha za serikali.

"Kwetu OSHA, imekuwa siku nzuri sana ambapo tumepata fursa ya kukutana na wajumbe wa kamati hii. Kama tunavyofahamu wabunge ni wawakilishi wa wananchi ambao ni wadau wetu hivyo kukutana nao na kujadiliana kuhusu masuala haya muhimu kutawezesha wadau wetu kupata elimu ya masuala haya kupitia wabunge katika majimbo yao," alisema Dk. Meru.

"Sisi kama watendaji tumefarijika sana kupata fursa ya kuwashirikisha waheshimiwa wabunge masuala haya ya usalama na afya mahali pa kazi kwa kuwa wao ndiyo wanaotunga sera na kuishauri serikali hivyo wakiyafahamu vyema majukumu yetu ndivyo watakavyoweza kuishauri vizuri serikali."

# 'Wataalamu acheni kulalamika toeni huduma bora'

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

WIZARA ya Afya imewataka wataalamu wa afya hapa nchini kuondoa malalamiko kwa wananchi kwa kutoa huduma bora za afya.

Katibu Mkuu wa wizara hiyo, Prof. Abel Makubi, alitoa kauli hiyo mwishoni mwa wiki kwenye kikao na Waganga Wakuu wa Wilaya na Wafawidhi kilichofanyika kwa njia ya mtandao na kushirikisha wakurugenzi kutoka idara na vitengo vya wizara hiyo.

Aliwataka kufuata misingi, miongozo na taaluma zao wakati wa utoaji huduma ikiwamo matumizi ya lugha nzuri kwa wateja wanaofika kupata huduma ili kuondoa malalamiko kwa wananchi yanayozuilika.

"Hakuna kitu kinachotia hasira kama vitu vidogo vidogo kushindwa kufanyika katika maeneo ya kutolea huduma, mfano suala la lugha mbaya kwa wananchi wanapoenda kupata huduma, hii ni lazima muifanyie kazi," alisema. "Nitoe wito kwenu, kila mtu atimize wajibu wake katika utendaji ili kuleta matokeo chanya katika sekta ya afya, hili liendane na ubunifu na uchapaji kazi ili tuone mabadiliko katika vituo vyenu vya utoaji huduma." Alisema wizara imejipanga kusimamia utekelezaji wa mwongozo wa ukaguzi wa kliniki kwenye vituo vya kutolea huduma za afya ili kuboresha huduma na kuleta matokeo chanya kwa wananchi.

Kadhalika, Prof. Makubi aliwataka wataalamu hao kusimamia huduma za mama na mtoto katika maeneo yao ili kuondoa vifo vya wajawazito.

Aliagiza kusimamia vizuri fedha za wadau na za serikali zinazopelekwa katika vituo vyao. Naye Naibu Katibu Mkuu anayesimamia masuala ya afya kutoka Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Dk. Grace Magembe, alisema katika bajeti ya mwaka 2022/23, ofisi hiyo imeweka kipaumbele kikubwa kwenye vifaa tiba, kuajiri watumishi, kujenga na kukarabati hospitali mpya za wilaya na zahanati ili kuboresha huduma kwa wananchi.





## DC Kyela awataka kubuni vyanzo vya mapato

**Na Grace Mwakalinga,** KYELA

MKUU wa Wilaya ya Kyela, Ismail Mlawa, ameliomba Baraza la Madiwani wilayani humo, kusaidia kubuni vyanzo vya mapato kwa lengo la kupata fedha kukamilisha miradi ya maendeleo.

Mlawa alitoa kauli hiyo mwishoni mwa wiki kwenye kikao cha madiwani, kuwa kwa sasa wilayani hiyo haina vyanzo vya kutosha vya kukusanya mapato hali inayochangia baadhi ya miradi kutokukamilika kwa wakati.

"Kutokana na upungufu wa vyanzo vya mapato na kusuasua kwa miradi inayojengwa kwa kutegemea mapato ya ndani, madiwani waisaidie kutafuta ili kupata fedha za ujenzi wa miradi kama vile vituo vya afya na shule," alisema Mlawa.

Aidha, aliwakumbusha watendaji wa halmashauri hiyo, kukusanya ushuru kwa kuzingatia haki na uaminifu na kwamba mtumishi yeyote atayebainika kujiingiza kwenye vitendo vya rushwa atachukuliwa hatua kwa mujibu wa sheria.

Alisema ni lazima mtumishi wa umma azingatie maadili ya kazi kwa kuhakikisha anatimiza wajibu wake ipasavyo wa kuwahudumia wananchi na miongoni mwa majukumu hayo ni pamoja na ukusanyaji wa kodi halali.

Mkurugenzi wa halmashauri ya wilaya hiyo, Ezekiel Magehema, alisema hadi sasa vituo vya afya vinne vimejengwa kati ya hivyo wiwili vimekamilika na kuanza kutumika na vingine vikiwa kwenye hatua za mwisho za kukamilisha.

Alisema ujenzi wa vituo hivyo unategemea mapato ya ndani na ili kukamilisha mradi mingi lazima kuwapo na vyanzo vingi vya mapato ndani ya halmashauri ili kurahisisha shughuli za ujenzi wa miradi.

Diwani wa Viti Maalum wilayani humo, Tumaini Mwakatika, alisema wao ni sehemu ya halmashauri wataendelea kutoa ushauri na mapendekezo ya kupata vyanzo vingine vya mapato.

Alisema kwa kuwa wanaishi na wananchi na wanajua mazingira yao suala hilo ni rahisi na watakuja na mkakati wa kuhakikisha wilaya hiyo inakusanya fedha nyingi na kukamilisha miradi wanayoikusudia.



Salma Mdaki wa Jukwaa la Wanawake akipokea cheti cha pongezi kwa Ofisa Biashara wa Jiji la Dodoma, Donatila Donisi, baada ya kushiriki mafunzo ya kujiinua kiuchumi yaliyofanyika juzi Dodoma. (Kulia) Ofisa Masoko wa Jiji, Getrude Lumambo na Mwenyekiti wa Jukwaa la Wanawake (wa pili kushoto), Mary Mabhaye. **PICHA: PETER MKWAVILA**

## Madiwani wachukizwa kuchelewa jengo kuhudumia wagonjwa corona

**Na Grace Mwakalinga,** CHUNYA

MADIWANI wa Halmashauri ya Wilaya ya Chunya, mkoani Mbeya, wamechukizwa na kitendo cha Ofisi ya Mganga Mkuu wa wilaya hiyo kuchelewa kukamilisha ujenzi wa jengo la kuhudumia wagonjwa wa corona licha ya serikali kutoa fedha.

Walieleza hali hiyo mwishoni mwa wiki kwenye kikao cha Baraza la Madiwani walipokuwa wanapitia taarifa ya kamati ya fedha.

Diwani wa Viti Maalum wilayani humo, Phide Mwalukasa, alihoji mbele ya baraza hizo sababu za kusuasua kwa ujenzi wa jengo hilo katika Hospitali ya Wilaya ya Chunya licha ya serikali kutoa fedha kwa zaidi ya miezi mitatu sasa huku kukiwa hakuna majibu yasiyoridhisha.

Alisema haieleweki ni lini ujenzi utaanza na utakamilika ili wananchi waanze kupata huduma za vipimo na matibabu na kuomba Baraza kutoa uamuzi ili ujenzi huo ukamilike kwa kipindi kilichopangwa.

Akitoa ufafanuzi wa suala hilo, Kaimu Mganga Mkuu wa Wilaya ya Chunya, Edward Tengulaga, alisema ujenzi huo umekwama kutokana na kuhamishwa kwa eneo la awali ambalo lilitolewa ushauri na kamati ya fedha na baada ya kutakiwa kuanza kwa ujenzi ikagundulika kuwa mkandarasi hakuwa na vigezo.

"Hata hivyo baada ya kupitia vigezo mfumo wa fedha ulifungwa na kulazimika kusubiri hadi ufunguliwe, lakini sasa mchakato huo umeshafanyika hivyo ujenzi wa jengo hilo unatarajiwa kuanza wiki hii," alisema Tengulaga.

Akitoa maelekezo ya Baraza, Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Chunya, Bosco Mwanginde alisema ni mara nyingi Idara ya Afya haitekelezi maagizo na kwamba kuanzia kikao kijacho kama kutatokea uzembe wowote hakutakuwa na onyo zaidi ya kumchukulia hatua mkuu ya idara.

"Baraza la Madiwani linatoa onyo la mwisho kwa Mganga Mkuu wa wilaya, tukiona hakuna mabadiliko kikao kijacho kitatoa maazimio haiwezekani kila maagizo yanapuuzwa ina maanisha wanatudharau," alisema Mwanginde.

Mkuu wa Wilaya ya Chunya, Simon Mayeka, aliunga mkono kauli ya Mwenyekiti wa halmashauri na kumtaka Ofisa Utumishi kujitafakari kwa kufumbia macho upungufu unaojitokeza kwa watumishi na kushindwa kuwachukulia hatua.

"Kwa nini kila kikao tunaongea kuhusu idara ya afya, ifike muda tuanze kuchukua hatua pia Ofisa Utumishi ujitathmini inawezekana unayajua mapungufu haya, lakini unakaa kimya maovu yanatendeka wewe upo pia mkurugenzi yupo sasa inatosha," alisema Mayeka.

Mbunge wa Jimbo la Lupa, Masache Kasaka, aliwataka watendaji wa halmashauri kuwasaidia madiwani kutekeleza majukumu yao kwa kuzingatia kanuni na sheria za utumishi ili wilaya hiyo iweze kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo.

## CST yaomba vyuo ualimu vitoe mafunzo maalum wenye uhitaji

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

SHIRIKA la Child Support Tanzania (CST), linalojihusisha na kuhamasisha utoaji wa elimu jumuishi kwa shule mbalimbali za msingi jijini hapa, limeomba serikali kuhakikisha vyuo vyote vya walimu vinatoa mafunzo maalum ya namna ya kufundisha watoto wenye mahitaji maalumu ili wanapohitimu wawe na ujuzi pamoja na utayari wa kufundisha kundi hilo kuliko ilivyo sasa wanalazimika kupata mafunzo upya.

Ombi hilo lilitolewa mwishoni mwa wiki na Mkurugenzi wa CST, Noela Msuya, alipozungumza na Nipashe namna wanahakikisha wanahudumia watoto wenye mahitaji maalum kupitia programu ya elimu jumuishi.

Msuya alisema licha baadhi ya vyuo vya walimu kutoa mafunzo kwa ajili ya kuwafundisha watoto wenye mahitaji maalum, uhitaji ni mkubwa na serikali haina budi kutoa mafunzo hayo kwa vyuo vyote vya walimu nchini ili kuwasaidia watoto wenye ulemavu kusoma kwenye mazingira mazuri kupitia elimu jumuishi.

Alisema kutokana na uhaba wa walimu wa kufundisha watoto wenye mahitaji maalum kupitia mpango wa elimu jumuishi CST imekuwa ikitoa mafunzo maalum kwa walimu namna ya kuwafundisha watoto hao.

"CST tumejikita kuwahudumia watoto wenye ulemavu nchini ni baada ya kuona wanapata vikwazo mbalimbali ikiwamo kufungiwa ndani na kukosa haki ya kupata elimu, matibabu na huduma nyingine kupitia programu yetu ya peleka marafiki zangu wote shule tumeweza kuwafikia watoto wengi," alisema Msuya.

Aliongeza kuwa hadi sasa jumla ya watoto 600 wamefikiwa na programu hiyo kupitia shule 30 za msingi mkoani hapo na lengo lao ni kuzifikia shule zote nchini.

Kaimu Katibu Tawala wa Mkoa wa Mbeya, Vicent Mbua, aliwataka wananchi kutoa taarifa kwa serikali dhidi ya wanaowaficha watoto wenye ulemavu ndani.

Alisema yeyote atakayebainika hatua kali za kisheria zitachukuliwa dhidi yake na kwamba lengo la msisitizo huo ni kuwahakikisha watoto wenye ulemavu wanapata haki ya elimu kama walivyo wengine.

Aidha, alilishukuru CST kwa kujikita kuwasaidia watoto wenye ulemavu kwa kuanzisha shule yao yenye mahitaji maalum pamoja na kuendesha programu mbalimbali zinazohamasisha kuwapeleka watoto wenye ulemavu shuleni.

Alisema serikali inaendelea kuboresha miundombinu ya elimu inakuwa rafiki kwa watoto wenye ulemavu na utekelezeaji unaendelea hata sasa kupitia ujenzi wa vyumba vya madarasa baada ya fedha za UVIKO-19 kutolewa na serikali mbalimbali nchini.

Mwalimu anayehudumia watoto wenye mahitaji maalum, Shule Msingi Katumba II, Juma Said alisema CST imekuwa na mchango kubwa katika kutimiza ndoto za watoto wenye ulemavu.

Alisema shule yao inafanya kazi kwa karibu na CST na wanapata msaada wa vitu mbalimbali ikiwamo ujenzi wa miundombinu madarasa pamoja na vifaa mbalimbali vya kufundishia na kujifunzia.

Alisema kutokana na maboresho ya miundombinu ya majengo na vifaa yanayotolewa na serikali kwa kushirikiana na wadau kama CST ongezeko la kudahili wanafunzi limekuwa likiongezeka mwaka hadi mwaka kutoka wanafunzi 50 hadi 70.



# Mwinyi aishukuru Taasisi Uturuki kuitambua Z'bar

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, ameishukuru Taasisi ya Iyilik Dernegi kutoka nchini Uturuki kwa azma yake ya kuifanya Zanzibar kuwa kituo kikuu cha kuandaa utekelezaji wa miradi yote kwa nchi za Afrika Mashariki.

Dk. Mwinyi aliyasema hayo Ikulu Zanzibar, alipozungumza na ujumbe wa Taasisi ya Iyilik Dernegi ulioongozwa na Kaimu Mwenyekiti wake Metin Calbay, kuhusu shughuli zinazofanywa na taasisi hiyo katika nchi mbalimbali barani Afrika na Mashariki ya Kati.

Alisema amefurahishwa na azma ya taasisi hiyo ya kuifanya Zanzibar kuwa kituo kikuu kwa miradi yote inayotekelezwa na taasisi hiyo kwa nchi za Afrika Mashariki na kwamba serikali itatoa kila aina ya ushirikiano kufanikisha azma hiyo.

Alisema serikali imepokea ombi la taasisi hiyo la kupatiwa eneo la ardhi kwa ajili ya ujenzi wa kituo hicho kitakachohusisha majengo ya shule kuanzia ngazi ya maandalizi hadi sekondari, chuo cha kilimo pamoja na chuo cha ufundi.

Alieleza kufurahishwa na misaada inayotolewa na taasisi hiyo kwa jamii ya Wazanzibar na barani Afrika kwa kutambua kuwa jukumu hilo ni kazi ya serikali.

Naye Kaimu Mwenyekiti, Metin Calbay, alisema taasisi hiyo ina azma ya kujenga kituo kikuu Zanzibar kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya kudumu katika nchi za Afrika Mashariki na kuiomba serikali kuangalia uwezekano wa kupatiwa eneo hilo ili kufanikisha jambo hilo.

Alisema ujenzi wa kituo hicho utahusisha majengo ya shule, chuo cha kilimo, chuo cha ufundi na mradi huo utaanza eneo hilo litakapopatikana.

Alisema taaisisi hiyo imeshawasaidia wananchi wa Zanzibar mbuzi 450 wa maziwa, mbuzi 1,550 kwa ajili ya wananchi wa Tanzania Bara ikiwa ni hatua ya kuwawezesha kiuchumi.

Alisema taasisi hiyo pia hutoa misaada katika uchimbaji wa visima na kutoa misaada katika maeneo yanayokumbwa na majanga ikiwamo vita.

Pia imefanikisha ujenzi wa nyumba na shule kwa wakimbizi walioko katika maeneo yenye vita nchini Syria na kusaidia mbuzi milioni tatu wa maziwa kwa nchi 25 barani Afrika ikiwa ni hatua ya kusaidia familia zenye maisha duni.



Spika wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar, Zubeir Ali Maulid (kulia), akipokea Ripoti ya Ukaguzi wa Hesabu za Serikali ya mwaka 2020/2021 kwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora Zanzibar, Haroun Ali Suleiman, katika hafla iliyofanyika Chukwani. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Serikali kuwezesha wajasiriamali kiuchumi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi, Suleiman Masoud Makame, amesema lengo la serikali ni kuwawezesha wajasiriamali kiuchumi kuchochea na kusaidia upatikanaji wa ajira kwa vijana kupitia matumizi endelevu ya rasilimali za bahari nchini.

Alisema hayo jana Mjini Zanzibar katika kikao cha uwasilishwaji wa ripoti ya mrejesho kuhusu maagizo na maelekezo yaliyotolewa hivi karibuni na Kamati ya Uchumi wa Buluu ya Baraza la Wawakilishi.

Waziri Suleiman alisema Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi imeanza mchakato wa ujenzi wa kiwanda cha kusarifu mwani kilichoko Chamanangwe Pemba kwa ajili ya kukuza pato la taifa hasa kwa wakulima wa zao la mwani pamoja na ongezeko la mnyororo wa thamani wa ajira kupitia zao hilo. "Serikali imeamua kutoa vifaa kwa wakulima wa zao la mwani kwa ajili ya kuinua bei ya mwani mkavu aina ya spinosum ambao ulikuwa ukinunuliwa kwa shilingi 600 bei ambayo hailingani na hali ya kiuchumi, hivyo jitihada zinaendelea kufanyika kupitia wizara hii kwa sasa umefikia kilo shilingi 1200," Suleiman alisema.

Aidha, alisema ni dhahiri kuwa rasilimali za bahari ndiyo mkombozi wa taifa la Zanzibar kutokana na usafirishaji wa zao la mwani kipekee nje ya nchi umeongezeka kwa kiasi kikubwa kutoka tani 11,383 mwaka 2020 hadi 12,124 mwaka 2021 sawa na ongezeko la asilimia 6.1.

Alisema zimejitokeza kampuni mbalimbali kwa ajili ya kutoa vifaa vya uokotaji wa mwani aina ya Ulva (mafusho) ambao kwa kuanzia utanunuliwa kwa kilo Sh. 800 ukiwa mkavu.

"Wizara ina mpango wa kutoa mafunzo hivi karibuni kwa wananchi wa Zanzibar jinsi ya kuokota na kuanika mwani huo ambao uliokua ukitumika kama dawa ya kufusha watoto ambao kwa sasa umekua biashara badala ya kuzagaa katika fukwe za bahari," alisema.

Kadhalika, alisema wizara yake imejipanga kutoa masanduku ya kuhifadhia barafu na samaki pamoja na meza ndogo za kinamama wanaouza samaki katika sinia ili kuimarisha uchumi wa buluu nchini.

Mwenyekiti wa Kamati ya Uchumi ya Baraza la Wawakilishi, Sabiha Filifili Thani, aliipongeza wizara hiyo kwa kutekeleza yote ambayo yameagizwa na kamati hiyo ili kuenda sambamba na azma ya serikali katika kuwainua wananchi kiuchumi kupitia uchumi wa buluu.

Mjumbe wa kamati hiyo, Panya Ali Abdallah, alishauri Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi kuendelea kutafuta wafadhili kwa ajili ya kuongeza wataalamu ili kufanikisha shughuli za utafutaji na uchimbaji wa mafuta na gesi asilia.

# Saratani shingo ya kizazi tishio wanawake visiwani

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

UGONJWA wa saratani ya shingo ya kizazi unaendelea kuwaathiri wanawake wengi visiwani.

Akizungumza jana katika mkutano na waandishi wa habari kuhusu elimu ya kinga ya ugonjwa huo kwa wanawake, Mratibu wa Kitengo cha Maradhi yasioambukiza kutoka Hospitali ya Mnazi Mmoja, Omar Abdalla Ali, alisema idadi ya wagonjwa wanaougua ugonjwa huo inaongezeka kwa kasi kubwa.

Alisema saratani ya shingo ya kizazi inazuilika au kutibika endapo itagundulika mapema ikiwa kwenye hatua za awali na kwamba ni muhimu wananchi wakajichunguza afya mara kwa mara na kufuata ushauri wa wataalamu wa afya.

Alisema wanawake wote walio na umri wa miaka 30 na kuendelea, wanatakiwa kufanya uchunguzi wa saratani ya shingo ya kizazi kwa mwaka mara moja kwa kuwa wako katika hatari ya kupata ugonjwa huo.

Aliwataka kuacha kutumia kemikali za aina yoyote kuweka katika sehemu zao za siri jambo ambalo huathiri njia ya kizazi na kusababisha saratani ya shingo ya kizazi.

Naye Meneja wa Muungano wa watu wanaoishi na maradhi yasiyoambukiza Zanzibar (NCDs), Haji Khamis Fundi, aliitaka jamii hasa wanawake kufanya uchunguzi na kuachana na vichocheo vinavyosababisha maradhi hayo.

Alisema kukosekana elimu ya kujiepusha na saratani kwa jamii kunachangia kuwapo na kesi nyingi za ugonjwa huo na kushauri jamii kujiepusha na vichocheo vya maradhi hayo.

Aliitaka jamii kuacha matumizi ya vyakula vyenye kemikali nyingi na vya kwenye makopo vilivyopita muda wa matumizi, tumbaku, sigara, pombe na utiaji wa vitu visivyofaa sehemu za siri pamoja na matumizi ya mionzi ya mara kwa mara.

MAKALA MAALUM

# ‘Uzingatiaji Sheria Serikali Mtandao, msingi matumizi bora ya TEHAMA’

Na Mwandishi Maalum

UTEKELEZAJI wa Serikali Mtandao unategemea kuwapo kwa sera, sheria, kanuni, miongozo na mikakati madhubuti ili kuongoza utekelezaji sahihi na kulinda maslahi ya utekelezaji na watumiaji wa huduma zitolewazo na serikali kupitia Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA).

Sheria ya Serikali Mtandao Na 10 ya mwaka 2019 inaelekeza Taasisi za Umma nchini kuzingatia matakwa ya sheria na kuishirikisha Mamlaka ya Serikali Mtandao kabla ya kuanzisha au kujenga mifumo na miundombinu ya TEHAMA ili kuepuka urudufu wa jitihada za Serikali Mtandao.

Sheria nyingine zinazoratibu matumizi sahihi ya TEHAMA ni pamoja na Sheria ya Miamala ya Kielektroniki, 2015 (Electronic Transactions Act, 2015) na Sheria ya Makosa ya Mitandao, 2015 (Cybercrimes Act, 2015). Sheria hizi zinalenga kuimarisha udhibiti na kuboresha utekelezaji wa masuala yanayohusu TEHAMA nchini.

Sheria ya Serikali Mtandao inazitaka Taasisi za Umma kuwasiliana na Mamlaka ya Serikali Mtandao (eGA) kabla ya kujenga au kuanzisha mradi wowote wa TEHAMA. Hii ina maana kwamba taasisi inawajibu wa kutoa taarifa ya kuanzishwa kwa mfumo wowote au miundombinu ya TEHAMA kwenye taasisi husika.

Kwa mujibu wa sheria hii, mamlaka ina jukumu la kutoa ushauri wa kuendelea kwa mradi husika na kuitaka taasisi hiyo kutoa taarifa ya utekelezaji mara kwa mara. Aidha, miradi yote inatakiwa kuripotiwa kupitia mfumo wa Government ICT Service Portal (GISP).

Pia, sheria inasisitiza kujenga na kusimamia mifumo kwa kutumia wataalamu wa ndani, haya yote yanafanyika ili kuwawezesha wananchi kupata huduma mahali popote bila kujali muda.

Aidha, ili kuhakikisha Utekelezaji wa Sheria ya Serikali Mtandao hasa katika ujenzi wa miundombinu ya TEHAMA unafanyika katika viwango vinavyotakiwa, serikali imetengeneza miongozo na viwango vya utekelezaji ili kuhakikisha kuwa Taasisi za Umma zinatekeleza jitihada hizo katika viwango na ubora unaotakiwa.


Benedict Ndomba

Miongozo hiyo hulenga kutoa maelekezo kwa watekelezaji kufuata utaratibu sahihi katika matumizi ya TEHAMA serikalini. Miongozo hiyo inatoa pia maelekezo na ufafanuzi wa taratibu zinazotakiwa kufuatwa katika utekelezaji wa juhudi mbalimbali zinazohusu TEHAMA katika taasisi za umma.

Dhana ya Serikali Mtandao imejengwa katika nguzo kuu nne ambazo ni Sera, Sheria na Kanuni; Usimamizi na Utawala; Mifumo Tumizi na Miundombinu. Nguzo ya kwanza ya usimamizi ndiyo inayosimamia uwapo wa Sera, Sheria, Kanuni na Miongozo.

Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Serikali Mtandao, Mhandisi Benedict Ndomba, anasema ili Teknolojia ya Habari na Mawasiliano itumike serikalini lazima kuwe na usimamizi. Uwapo wa nguzo hii hutoa mwelekeo wa kuhakikisha teknolojia hii ya habari inayotumika serikalini inaratibiwa na kuainisha matumizi sahihi ya TEHAMA katika Taasisi za Umma.

Vilevile, Ndomba amesema kuwa, taasisi zote za umma nchini hazina budi kuzingatia kanuni, viwango na miongozo ya Serikali



Mtandao katika utendaji kazi wao ili kujenga mifumo yenye tija.

Aidha, anabainisha kuwa, sheria inazitaka na kuzielekeza taasisi za umma kuwasiliana na mamlaka ili kushirikiana na kuhakikisha matumizi ya TEHAMA yanakuwa yenye tija kwa taasisi husika na serikali kwa jumla.

“Mamlaka ya Serikali Mtandao ipo kwa ajili ya kuhakikisha matumizi ya TEHAMA serikalini yanakuwa yenye tija na faida kwa serikali na wananchi sio kwa ajili ya kuzibana taasisi za umma au kuzuia matumizi ya TEHAMA,” alisisitiza.

Naye Meneja wa Huduma za Sheria Mamlaka ya Serikali Mtandao, ACP Raphael Rutaihwa anasema, uwapo wa Sheria ya Serikali Mtandao na kanuni zake unasaidia kuwezesha matumizi sahihi ya TEHAMA katika taasisi za umma yanayoboresha utendaji kazi na kutoa huduma bora zinazopatikana kwa urahisi na haraka na kuwa na serikali ya kidigitali iliyo imara na endelevu.


ACP Rutaihwa anasema Sheria ya Serikali Mtandao inazitaka na kuelekeza kuwa taasisi za umma zinazohusika na ujenzi wa miundombinu ya serikali kama barabara, reli na majengo kuhakikisha kuwa yanawekewa mazingira wezeshi kwa ajili ya kupitisha miundombinu ya TEHAMA kuanzia wakati wa kuandaa michoro ya ujenzi wa miundombinu hiyo.

Pia ameongeza kuwa, kulingana na Sheria ya Serikali Mtandao taasisi za umma zinatakiwa kuwasilisha mapendekezo na nyaraka zote zinazohusu miradi ya TEHAMA kabla ya kuanza utekelezaji kwa ajili ya kuhakikiwa na kupitishwa na Mamlaka na baadaye kuwasilisha taarifa za maendeleo ya utekelezaji pamoja na taarifa ya mwisho baada ya kukamilika kwa mradi husika.

Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA) ni taasisi ya umma iliyoanzishwa kwa Sheria ya Serikali Mtandao Na. 10 ya mwaka 2019. Mamlaka ina jukumu la kuratibu, kusimamia na kukuza jitihada za Serikali Mtandao pamoja na kuhimiza utekelezaji wa Sera, Sheria, Kanuni, Viwango na Miongozo ya Serikali Mtandao kwa taasisi za umma.

Kuanzishwa kwa mamlaka hii mwaka 2019 kunaendeleza afua za Wakala ya Serikali Mtandao (eGA) iliyoundwa Aprili 2012 kwa Sheria ya Wakala za Serikali Na. 30 Sura ya 245 ya mwaka 1997 na kuchukua sehemu ya mipango yake kwa sababu majukumu ya taasisi hizi yanafanana ingawa yanatofautiana katika mamlaka ya utendaji.

Sheria ya serikali mtandao inapatikana kupitia tovuti ya mamlaka ya serikali mtandao ambayo ni www.ega.go.tz, tovuti ya Bunge ambayo ni Bunge.go.tz na online Tv ya Mamlaka eGA online TV.



## UN kuendelea kukagua kinu cha nyuklia cha Zaporizhzhia Ukraine

**LONDON,** UINGEREZA

WIZARA ya Ulinzi ya Uingereza imesema kwamba wataalamu wa nyuklia wa Umoja wa Mataifa wataendelea kukagua eneo la Enerhodar lililo Kusini mwa Ukraine kunapoelezwa kuwapo na kinu cha nishati ya nyuklia cha Zaporiazhzhia.

Taarifa hiyo pia ilieleza kuwa, timu ya wataalamu hao imemaliza ziara yake ya kwanza ya kutathmini usalama na ulinzi wa kinu cha Zaporizhzhia Alhamisi, licha ya mapigano kati ya majeshi ya Russia na Ukraine yanayoendelea karibu na mtambo huona wataendelea na kazi yao siku ya Ijumaa.

Wizara hiyo pia imeeleza katika taarifa yake kuwa mazoezi ya pamoja ya kimkakati ya Russia yaliyoanza Alhamisi iliyopita yamefeli kuhimili uwezo wa kijeshi kwa ngazi ya juu. Na kuwa matukio hayo yamesajiliwa kikamilifu, kimsingi yanakusudia kuwafurahisha viongozi wa Russia na watazamaji wa kimataifa.

Rais wa Ukraine Voldymyr Zelenskyy, kwenye hotuba yake Alhamisi iliyopita alisema kuwa Ukraine ilifanya kila njia kuhakikisha suala hilo hilo linafanyika. Jambo la kusikitisha ni kuwa wavamizi wanataka kuifanya ziara hiyo kuwa isiyozaa matunda lakini wanapambana kuzuia watu hao.

Aidha, Mkurugenzi Mkuu wa IAEA, Rafael Grossi, akiongoza ujumbe wa wakaguzi 14, aliwaambia waandishi wa habari kuwa shirika hilo linaweka uwepo wao wa kudumu katika mtambo mkubwa zaidi wa nyuklia.

"Ni dhahiri kuwa heshima ya eneo la kinu cha Zaporizhzhia imekiukwa mara kadhaa. Nina wasiwasi na nitaendelea kuwa na wasiwasi kuhusu kinu hiki. Wakaguzi wa UN waliwasili katika kituo cha nyuklia licha ya "kuongezeka kwa harakati za kijeshi", alisema Rafael.

Mashambulizi hayo yalilazimisha kufungwa kwa moja ya kinu cha nyuklia kabla ya kuwasili kwa wakaguzi hao, lakini Grossi alisema hawatisitisha uchunguzi huo kwa sababu kuna faida kubwa kuliko hasara.

"Tuna kazi muhimu sana ya kukamilisha.Tutaanza mara moja kufanya tathmini ya usalama wa hali ya kituo hicho cha umeme," alisema.

DW

# Marekani kutuma mjumbe maalum Ethiopia kutuliza vita

**Washington,** MAREKANI

MAREKANI inatarajia kutuma ujumbe maalum, Mike Hammer nchini Ethiopia kujaribu kumaliza mapigano mapya yaliyozuka katika Jimbo la Tigray na kuzisihi kusitisha mashambulizi na zishiriki mazungumzo ya amani.

Taarifa iliyotolewa na Wizara ya Mambo ya Nje ya Marekani ilisema kuwa kupitia kwa ofisa habari wa Ikulu ya Marekani, Karine Jean-Pierre , ilisema kuwa Mike Hammer, mwanadiplomasia wa muda mrefu na ambaye hushughulikia pia Sudan na Somalia ataanza ziara hiyo kuanzia jana hadi Septemba 15 .

"Tunalaani hatua ya Eritrea kujiunga tena kwenye machafuko hayo, mwendelezo wa mashambulizi ya wapiganaji wa Chama cha Ukombozi wa Watu wa Tigray (TPLF) na mashambulizi yanayofanywa na serikali ya Ethiopia," alisema Karine.

Karine alisema kuwa mapigano hayo yalianza tena wiki iliyopita katika jimbo hilo la kaskazini baada ya miezi mitano ya utulivu. Hali iliyoondoa matumaini ya kupatikana suluhisho la amani dhidi ya mzozo huo uliodumu kwa miaka miwili, huku ukisababisha migogoro ya kibinadamu ambapo maeneo mengi jimbo hilo yanakumbwa na njaa.

"Hakutakuwa na suluhisho la kijeshi katika machafuko hayo, pande zote sharti zijizuie na tunahimiza pande zote kusitisha vita, ili kuwezesha usafirishaji wa misaada na huduma za msingi kwa wanaohitaji," amesema Karine.

Wakati huo huo, Chama cha TPLF ambacho kilitawala siasa za Ethiopia kwa miaka mingi kimesema nchi jirani Eritrea kwa mara nyingine imetuma vikosi Tigray kufanya mashambulizi ya pamoja na vikosi vya Ethiopia.

Wakati Shirika la Kutetea Haki za Binadamu la Amnesty International limesema vikosi vya Eritrea viliwaua mamia ya raia Novemba, 2020 katika mji wa kale wa Axum, huku Waziri Mkuu wa Ethiopia Abiy Ahmed alikiri uwepo wa vikosi hivyo na kutangaza viondoke mara moja.

DW



Athari za mafuriko yanayoendelea nchini Pakistan yanayodaiwa kusababishwa na mabadiliko ya hali ya hewa. **PICHA: MTANDAO**

# Kimbunga chasababisha huduma masomo, usafiri kusitishwa China

**Shanghai,** CHINA

MIJI ya mashariki mwa China imesitisha huduma ya feri, masomo na safari za ndege nchini Japan Jumapili kufuatia kimbunga Hinnamnor, ambacho kina nguvu kubwa mwaka huu duniani, kikielekea Taiwan na Korea Kusini na Kaskazini.

Mji wa Shanghai umesitisha huduma za feri, zaidi ya maofisa polisi 50,000 wakisaidia shughuli za uokoaji na kuelekeza magari upande mwingine mbali na maeneo hatari huku shule zikikufungwa katika kitovu cha biashara cha mashariki cha Wenzhou.

Kituo cha ufuatiliaji wa hali ya hewa cha Hong Kong kimetabiri Hinnamnor kusogea polepole kuelekea kaskazini hadi bahari ya East China ikiwa na upepo wenye kasi ya kilomita 175 kwa saa .

Shughuli za kuwaondoa watu na kufutwa kwa safari za ndege zimeamriwa kufanyika katika kisiwa cha Okinawa kusini mwa Japan. Kimbunga hicho pia kinatarajiwa kuleta mvua kubwa katika Rasi ya Korea, kukiwa na uwezekano wa kutokea mafuriko.

Aidha kituo cha taifa cha hali ya hewa China kilitoa tahadhari ya kimbunga hicho jana asubuhi na kuonya kuwa mvua kubwa zitapiga kaskazini mashariki mwa Zhejiang, Shanghai na kisiwa kinachojitawala cha Taiwan.

Nchini Japan, kimbunga kilipiga Okinwa na visiwa vya karibu kwa mvua kubwa na upepo mkali sana, na kutishia mafuriko na kusimamisha zaidi ya safari za ndege 100 zinaingia katika visiwa hivyo na sehemu za kisiwa kikuu cha kusini cha Kyushu.

Picha za video katika televisheni ya Taifa ya Japan, (NHK) zilionyesha miti ikitikisika kwa nguvu kutokana na kimbunga, huku mvua zikinyesha kwa nguvu katika vibaraza pembeni ya barabara.

Katika kisiwa kikuu cha Okinawa, wazee wawili walianguka na kujeruhiwa kidogo, kulingana na taarifa za vyombo vya habari.

Maofisa wanasema kusogea polepole kwa kimbunga hicho kunaweza kuongeza kiwango cha mvua na hatari ya kuwepo mafuriko katika mji wa kusini ambapo mawingu mazito yalikuwa yametanda.

Nchini Taiwan, zaidi ya wakazi 600 huko katika kaunti za New Taipei, Taoyuan na Hsinchu waliondolewa na kupelekwa maeneo salama Jumamosi wakati mvua kubwa na upepo wenye kasi ukipiga, kulingana na Shirika la habari la Central News la kisiwa hicho.

Kimbunga hicho kilisababisha maporomoko ya ardhi katika kaunti ya Miaoli na kuangusha miti zaidi ya 100 iliyoko pembeni mwa barabara. Takriban safari 40 za ndege na zaidi ya huduma 100 za feri kote nchini Taiwan zilisitishwa Jumamosi.

# MANDONGA ULINGONI TENA KIDUKU AKIZICHAPA NA MMISRI

Na Saada Akida

ZIKIWA zimesalia takriban wiki mbili na 'ushee' kabla ya pambano la ngumi kuwania ubingwa wa UBO Afrika, kati ya Mtanzania Twaha Kiduku na Abdo Khaled kutoka Misri, maandalizi sasa yamefikia hatua nzuri.

Wababe hao wanatarajiwa kupanda ulingoni Septemba 24, mwaka huu, katika pambano kali lililopewa jina la 'Mtwara Ubabe Ubabe 2', ambalo litafanyika katika Uwanja wa Nangwanda Sijaona mkoani Mtwara.

Akizungumza na gazeti hili jana, Promota wa pambano hilo, Suleman Semunyu, alisema kila kitu kipo sawa na mambo yanaendelea vizuri Mtwara, ikiwamo usalama na maandalizi ya mabondia ambao watapanda ulingoni siku hiyo.

**Alisema matarajio makubwa ya pambano hilo ni kuvutia wadau wa masumbwi kwa sababu ya rekodi nzuri za mabondia hao, ambao ni mara ya kwanza kukutana ulingoni.**

"Kila kitu kinaenda vizuri, mbali na pambano la Kiduku na Khaled, pia kutakuwa na mapambano ya utangulizi kwa mabondia kutoka sehemu mbalimbali akiwamo Kareem Mandonga kupanda tena ulingoni," alisema.

Alisema katika mapambano ya utangulizi ya 'Mtwara Ubabe Ubabe 2', yatakuwa kati ya Nasra Msami dhidi ya Halima Bandora, Francis Miyeyusho atazichapa na Adam Lazoro na Selema Galileo dhidi ya Shaban Ndaro.

Wengine ni Alto Kyenga dhidi ya Ibrahim Tamba, Bosco Bakari atazichapa na Maliki Deo huku Joseph Mchapeni akipanda ulingoni kuzichapa na Pascal Manyota.

MAMBO MOTO...



Mjumbe wa Bodi ya Wakurugenzi wa Kampuni ya Multichoice Tanzania , Nehemiah Mchechu, akizungumza katika hafla maalumu iliyoandaliwa kwa ajili ya kuukaribisha msimu mpya wa michezo, burudani na sanaa kupitia DSTV,

# Dodoma Jiji macho kwa Singida Big Stars

Na Adam Fungamwango

KIKOSI cha Dodoma Jiji FC, kimerejea mazoezini kujiandaa na mechi ya raundi ya tatu ya Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Singida Big Stars inayotarajiwa kuchezwa Jumapili wiki hii kwenye Uwanja wa Liti mkoani Singida kwa tahadhari kubwa baada ya kupoteza mechi zote mbili za mwanzo.

Kocha Msaidizi wa klabu hiyo, Mohamed Muya, amesema wanaiangalia mechi hiyo kwa uzito mkubwa kwani matokeo yake yatawapa ramani ya malengo yao kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara msimu huu, huku akiamini wanakwenda kupata ushindi wa kwanza.

"Hatukuanza vizuri, tumerejea mazoezini, kazi yetu ni kuangalia makosa, tutajaribu kuangalia mapungufu yetu ili tuwe bora.

Kiu yetu ni kupata matokeo mazuri, kwa hiyo tunachofanya ni kujitathmini wapi tulikwama, kwenye fiziki tutafanyia kazi, kiufundi tutaangalia mfumo wetu sehemu gani ulikuwa na shida, tutaanza kwa kuongea nao, tutakwenda kwenye ubao na video kuangalia na baadaye tutarudi uwanjani," alisema kocha huyo.

Dodoma Jiji imeanza kwa rekodi mbaya msimu huu kwa kupoteza mechi zote mbili, ilianza Ligi Kuu kwa kuchapwa mabao 3-1, na ikakubali kipigo cha 2-1 dhidi ya Prisons.

Hata hivyo, inakwenda kucheza na timu ambayo imeshinda mechi zote mbili, ikiichapa Prisons bao 1-0 na ikashinda mabao 2-1 dhidi ya Mbeya City.

# Kisinda awasili rasmi Yanga

Na Hadija Mngwai

WAKATI kesho ikishuka dimbani kuivaa Azam FC, winga wa Yanga aliyerejea kikosini hapo akitokea RS Berkane ya Morocco, Tuisila Kisinda, ametua rasmi kujiunga na mabingwa watetezi hao.

Kisinda ambaye ni raia wa DR Congo aliwahi kuitumikia Yanga kabla ya kujiunga na RS Berkane kwa msimu mmoja na sasa amerejea tena baada ya klabu hiyo ya Morocco kuachana naye.

Akizungumza na Nipashe jana, Meneja wa Yanga, Walter Harison, alisema Kisinda tayari ameshatua nchini kujiandaa na ligi pamoja na mchezo wao dhidi ya Azam FC utakaopigwa kesho katika Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

"Winga wetu Kisinda tayari ametua leo (jana) alfajiri na ameshajiunga na wenzake kambini pale Avic Town Kigamboni, tayari kwa maandalizi ya ligi na mchezo wetu dhidi ya Azam.

"Kikosi chetu kipo vizuri, maandalizi yamekamilika kuelekea mchezo wetu dhidi ya Azam, wachezaji wote wapo vizuri hakuna majeruhi wapya zaidi ya Ngushi," alisema.

# Netiboli Tanzania 'yapoteana' Sauzi

Na Adam Fungamwango

TIMU ya netiboli ya Tanzania imeshindwa kufanya vema kwenye michuano ya kusaka tiketi ya kufuzu fainali za Kombe la Dunia baada ya kufungwa mechi zote nne, huku timu za Afrika Kusini na Malawi zikifuzu kucheza fainali hizo.

Habari kutoka Afrika Kusini ilikokuwa ikifanyika michuano hiyo kuanzia Agosti 17, mwaka huu, zimeeleza timu mwenyeji, Sauzi imetwaa Ubingwa wa Afrika kwa mchezo huo baada ya kuitwanga Malawi mabao 60-44 kwenye mechi ya fainali.

Tanzania iliyokuwa kwenye Kundi A katika michuano hiyo iliyofanyika Pretoria, Afrika Kusini, ilianza kwa kukung'utwa na Namibia mabao 47-46, ikachapwa 54-45 dhidi ya Botwana, ikafungwa 58-33 dhidi ya Afrika Kusini kabla ya kukandikwa mabao 43-33 na Zimbabwe.

Timu ya Afrika Kusini iliongoza Kundi A kwa pointi nane ikishinda mechi zote nne ilizocheza huku Kundi B, timu ya Malawi ikiongoza kwa pointi sita, ambapo ilikuwa na timu za Eswatini, Kenya, Zambia na Uganda.

## HABARI MICHEZO

### ZISIKUPITE

**SOUTHAMPTON NA LAVIA**

KLABU ya Southampton ilikataa ofa ya pauni milioni 50 kutoka kwa Chelsea kwa kiungo wa kati wa Ubelgiji, Romeo Lavia mwenye umri wa miaka 18. (***Daily Echo***)

**MAWAKALA WAIDAI UNITED**

KLABU ya Manchester United ipo katikati ya vita vya malipo ya pauni milioni 20, huku mawakala watatu tofauti wakidai kuwa ndio waliochangia kiasi kikubwa katika uhamisho wa Antony kutoka Ajax. (***Mail***)

**TIMBER AMSHUKIA VAN GAAL**

MLINZI wa Ajax na Uholanzi, Jurrien Timber mwenye umri wa miaka 21, amekashifu madai 'ya uwongo' kwamba bosi wa timu yake ya Taifa, Louis van Gaal alimshauri kuhamia Old Trafford. (***Mirror***)

**BARCA KUMRUDISHA GRIEZMANN**

BARCELONA wanachukua ushauri wa kisheria kuhusu mkataba wa mkopo wa Antoine Griezmann wa Atletico Madrid, huku wajibu wa kununuliwa kwa euro milioni 40 ukisababishwa iwapo atacheza dakika 45 au zaidi katika mechi 14. Mshambuliaji huyo wa Ufaransa mwenye umri wa miaka 31, bado hajaanza katika mechi yoyote msimu huu. (***Mundo Deportivo via 90min***)

**CAICEDO AANIKWA UNITED**

KLABU ya Manchester United ilikataa nafasi ya kumsajili kiungo wa kati wa Brighton na Ecuador, Moises Caicedo mwenye umri wa miaka 20 kwa pauni milioni 4.5 miezi 18 iliyopita. (***The Athletic***)

**MALINOVSKYI NA SPURS**

KLABU ya Tottenham Hotspur ilitaka kumsajili kiungo wa kati wa Atalanta na Ukraine, Ruslan Malinovskyi mwenye umri wa miaka 29 msimu huu, lakini klabu hiyo ya Italia ilikataa kumuuza. (***Fabrizio Romano***)

**DIAZ KUNUNULIWA LEEDS**

KLABU ya Leeds United inatayarisha ofa ya kumnunua mshambuliaji wa Blackburn na Chile, Ben Brereton Diaz mwenye umri wa miaka 23 Januari. (***Football Insider***)

**ERIKSEN NA DILI LA UTD**

KLABU ya Manchester United ilimpa mchezaji wa Denmark, Christian Eriksen dili la thamani ya pauni milioni 43 ili kuzuia nia ya klabu yake ya zamani ya Tottenham Hotspur wakati aliposajiliwa bila malipo msimu huu wa majira ya joto. (***Football Insider***)

**HAMILTON KUINUNUA UNITED**

BINGWA mara saba wa dunia wa Formula, One Lewis Hamilton amesema hajawasiliana na Sir Jim Ratcliffe kuhusu ofa ya kutaka kuinunua Manchester United. (***Manchester Evening News***)

**BERGE AANIKWA CHELSEA**

KLABU ya Chelsea ilionyesha nia ya kumsajili kiungo wa kati wa Sheffield United na Norway, Sander Berge mwenye umri wa miaka 24 katika siku ya mwisho ya kufungwa kwa dirisha la uhamisho. (***Sheffield Star***)

**LAMPARD ALISHAURIWA**

KOCHA wa zamani wa Tottenham Hotspur, Harry Redknapp amesema alimwambia mpwa wake, Frank Lampard amsajili Dele Alli. (***Talksport***)



# DONDOO ZA SOKA
## M[illegible]TI YA ULAYA




# TUCHEL ASIFU UAMUZI VAR, MOYES APONDA

## ●●● Ilikuwa faulo ya wazi kwa mlinda mlango, mwenzake asema hii ni 'kashfa na uozo'...

**LONDON,** England

THOMAS Tuchel amekiri kuwa alifarijika kwa maamuzi ya utata ya Teknolojia ya Kumsaidia Refa ya (VAR), katika ushindi wa mabao 2-1 wa Chelsea dhidi ya West Ham, Jumamosi.

**Chelsea walipata bao la ushindi dakika za lala salama kupitia kwa Kai Havertz, lakini West Ham walionekana kusawazisha dakika za majeruhi kwa Maxwel Cornet kufunga baada ya kipa Edouard Mendy kugongana na Jarrod Bowen.**

Lakini VAR ikalikataa bao hilo na kuipa Chelsea ushindi na Tuchel aliona kama haki imefanya kazi yake baada ya hali kama hiyo kutokea kwenye sare ya mabao 2-2 dhidi ya Tottenham Hotspur mwezi uliopita.

"Ilikuwa faulo ya wazi kwa mlinda mlango," alisema Tuchel akiiambia BBC Sport.

"Nilikuwa na mashaka kuhusu ile la kwanza (bao la kwanza la West Ham) - lakini sitaongea. Mara ya mwisho niliadhibiwa kwa faini kubwa. Unatoa maoni yako, halafu unatozwa faini."

"Kwa maoni yangu ile ilikuwa faulo. Sitatoa maoni tena, lakini kilichotokea dhidi ya Tottenham kilikuwa dhahiri, na mimi nililipa fedha nyingi kwa kutoa maoni, kwa hiyo sitafanya hivyo."

Kocha wa West Ham, David Moyes aliezea maamuzi ya VAR kama 'kashfa' na 'uozo', kabla ya Declan Rice hajaandika kwenye Twitter na kuongeza: "Hayo ni moja ya maamuzi mabaya zaidi ya VAR kufanywa tangu ifike kwenye mchezo."

Chelsea walimaliza mchezo kwa kumiliki mpira kwa asilimia 69, lakini wakipiga mashuti sawa na yale ya wapinzani wao.

SportPesa
LIVE IN PLA

MECHI KALI
MIDDLESBROUGH
VERSUS
SUNDERLAND
1 | 1.75
X | 3.55
2 | 4.40

PIGA *150*87#
Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
18+ 0764115588, 0677115588
0685115588 GBT:0249
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa



# GUARDIOLA APAGAWA MAN CITY KUTOKA SARE

**MANCHESTER,** England

KOCHA Pep Guardiola alisikitishwa na ukosefu wa umakini kwa Manchester City walipolazimishwa sare ya bao 1-1 na Aston Villa kwenye Ligi Kuu England, Jumamosi.

Man City walionekana kuelekea kileleni mwa jedwali wakati Erling Haaland alipofunga bao la kuongoza dakika tano baada ya kipindi cha pili.

Mshambuliaji huyo wa zamani wa Borussia Dortmund sasa amefunga mabao 10 katika mechi zake sita za kwanza za Ligi Kuu England - akiwa mchezaji mwenye kasi zaidi kufikisha mabao hayo, tangu Mick Quinn alipofanya hivyo Desemba, 1992.

Pia ni mchezaji wa tano kufunga katika kila mechi kati ya mechi tatu za kwanza ugenini kwenye Ligi Kuu England, baada ya Peter Beardsley, Jurgen Klinsmann, Francesco Baiano na Alen Boksic.

City walipoteza nafasi nyingi za kuendeleza faida yao baada ya bao la kwanza la Haaland, na kumwacha Guardiola akikasirika kwa uzembe wa timu yake.

"Ulikuwa mchezo mzuri. Tuliruhusu bao moja tu kutoka kwa shuti moja lililolenga goli ndani ya dakika 90," alisema Guardiola akiiambia Sky Sports.

"Hatukuwa sahihi katika miguso yetu ya tatu ya mwisho na mambo yetu rahisi, haswa kipindi cha kwanza. Tulipata nafasi ya kufunga la pili wakati mchezo ukiwa mikononi mwetu, lakini hatukufanya hivyo.

"Tulikuwa bora baada ya bao, lakini hatukuwa sahihi vya kutosha kwenye krosi; tulikosa hali chache na ndiyo maana hatukuweza kufunga.

"Walilinda vema, walijipanga vema. Tulitengeneza nafasi za kutosha za kufunga mabao na tulijilinda vema mbali na hatua moja."

# Xavi: Ushindi Barca kwa Sevilla ni ishara nzuri

**BARCEONA,** Hispania

XAVI amesema namna Barcelona walivyoshinda mabao 3-0 dhidi ya Sevilla kwenye Ligi Kuu Hispania, LaLiga ni "ishara nzuri" kwao.

Raphinha alianza kwa kufunga bao lake la kwanza kwa Barca na bao la tano kwa Robert Lewandowski katika michezo mitatu ya LaLiga likaongeza uongozi wao mara mbili katika kipindi cha kwanza.


Eric Garcia aliongeza faida yao kwa bao lake la kwanza kwa timu hiyo pale kwenye dimba la Ramen Sanchez-Pizjuan, ambapo Jules Kounde alitoa pasi mbili za mabao dhidi ya klabu yake ya zamani.

Mashabiki wa Sevilla waliojawa na hasira waliizomea timu yao kufuatia kipigo kilichowafanya wabaki na pointi moja pekee katika mechi nne, huku Barca wakiwa nafasi ya pili nyuma ya Real Madrid baada ya ushindi wa tatu mfululizo.

Miamba hiyo ya Katalunya imefunga mabao 11 katika mechi tatu na timu yenye sura mpya inaonekana kama inaweza kuwa bora zaidi msimu huu.

Mara baada ya mchezo huo, Kocha mkuu wa Barca, Xavi alisema: "Tumekuwa na nafasi za kufunga mabao zaidi. Ni ishara nzuri kuja Sevilla na kujituma, timu iko katika wakati mzuri sana."

Ousmane Dembele aliisababishia timu dhaifu ya Sevilla matatizo ya kila aina kabla ya kutolewa kipindi cha pili na Xavi ambaye alifurahishwa na matokeo ya winga huyo.



"Najua Ousmane ana uwezo gani, ni mchezaji ambaye tabia yake naipenda sana, si tu katika ushambuliaji bali pia katika safu ya ulinzi," alisema.

CHEZA USHINDE KASINO

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!

SPORTPESA APP

PAKUA APP YETU, BET LEO UWE MILIONEA

MECHI ZA USHINDI

"1" - NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
"X" - NI TIMU KUTOKA SARE
"2" - NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMATATU - 05/09/2022

| MUDA | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:00 | 5248 | Seoul E Land vs Gyeongnam | 2.64 | 3.33 | 2.38 |
| 13:30 | 4968 | Anyang vs Jeonnam Dragons | 1.74 | 3.53 | 4.11 |
| 16:00 | 4167 | Kairat Almaty vs Tobol Kostanay | 2.41 | 3.13 | 2.74 |
| 17:00 | 5220 | Aktobe vs FK Kyzylzhar Petropavlovsk | 1.57 | 3.63 | 5.30 |
| 17:30 | 1110 | Aluminium Arak vs Teraktor Sazi | 2.60 | 2.55 | 3.09 |
| 18:00 | 1149 | Loko Tbilisi vs Dila Gori | 9.63 | 5.31 | 1.24 |
| 18:00 | 2919 | Astana vs Akzhaiyk Uralsk | 1.28 | 4.81 | 9.23 |
| 18:00 | 2940 | HJK Helsinki vs Hifk | 1.15 | 6.46 | 12.72 |
| 18:00 | 5113 | Havadar vs Persepolis FC | 6.31 | 3.25 | 1.58 |
| 18:00 | 5952 | FK Auda vs BFC Daugavpils | 1.49 | 4.04 | 5.52 |
| 18:30 | 3556 | Al Qadisiyah vs Al Orubah | 2.05 | 3.05 | 3.80 |
| 19:00 | 2067 | Stabaek vs Bryne | 1.30 | 5.10 | 7.26 |
| 19:00 | 2324 | Radnik Surduluca vs Cukaricki St | 4.63 | 3.45 | 1.68 |
| 19:00 | 2810 | Peka vs PPJ | 2.80 | 3.92 | 2.05 |
| 19:00 | 2846 | Sogndal vs Skeid Fotball | 1.74 | 3.69 | 3.93 |
| 19:00 | 3937 | Hapoel Rishon Lezion vs AS Ashdod | 2.24 | 3.13 | 3.28 |
| 19:00 | 4483 | Raufoss vs Fredrikstad | 2.19 | 3.50 | 2.81 |
| 19:00 | 5263 | Grorud IL vs Ranheim | 3.82 | 3.87 | 1.72 |
| 19:00 | 5530 | Hapoel Petah Tikva vs Hapoel Kfar Saba | 2.18 | 3.03 | 3.54 |
| 19:30 | 1120 | Foolad Khuzestan vs MES Rafsanjan | 2.30 | 2.65 | 3.75 |
| 19:30 | 3638 | Zob Ahan vs Sepahan Esfahan | 4.63 | 3.01 | 1.81 |
| 19:30 | 4329 | Salernitana vs Empoli | 2.19 | 3.26 | 3.16 |
| 19:30 | 4555 | Monza vs Atalanta | 5.21 | 4.11 | 1.55 |
| 20:00 | 1298 | IFK Varnamo vs Helsingborg | 1.92 | 3.34 | 3.59 |
| 20:00 | 1584 | Samsunspor vs Manisa BBSK | 1.84 | 3.44 | 3.78 |
| 20:00 | 1907 | IK Brage vs Utsiktens BK | 2.43 | 3.36 | 2.85 |
| 20:00 | 1943 | Mjallby vs IFK Goteborg | 2.37 | 3.00 | 2.90 |
| 20:00 | 2556 | Torpedo Moscow vs Rostov | 3.70 | 3.40 | 1.94 |
| 20:00 | 3984 | Dalkurd FF vs Brommapojkarna | 3.77 | 3.72 | 1.90 |
| 20:00 | 4194 | Tondela vs CF Estrela | 2.11 | 3.18 | 3.38 |
| 20:00 | 4393 | Kalmar vs Varbergs Bois | 1.54 | 3.82 | 5.29 |
| 20:00 | 5049 | Aarhus vs Nordsjalland | 2.34 | 3.36 | 2.85 |
| 20:00 | 5856 | Paris 13 Atletico vs Sedan | 2.69 | 2.99 | 2.64 |
| 20:10 | 2467 | Norrkoping vs Hammarby | 3.39 | 3.49 | 1.93 |
| 20:15 | 5210 | Maccabi Netanya vs Hapoel Tel Aviv | 1.86 | 3.39 | 3.74 |
| 21:00 | 1089 | Jong Ajax vs Heracles Almelo | 2.72 | 3.71 | 2.23 |
| 21:00 | 1667 | Jong AZ Alkmaar vs Dordrecht | 1.68 | 3.98 | 4.18 |
| 21:00 | 2233 | Boavista vs Pacos Ferreira | 1.94 | 3.27 | 3.93 |
| 21:00 | 4317 | Galatasaray vs Gaziantep BB | 1.57 | 3.87 | 5.62 |
| 21:00 | 5192 | Jong PSV vs FC Oss | 1.85 | 3.68 | 3.68 |
| 21:30 | 1066 | Universitatea Craiova vs Farul Constanta | 2.13 | 3.21 | 3.36 |
| 21:30 | 1105 | Wisla Plock vs Gornik Zabrze | 2.04 | 3.38 | 3.19 |
| 21:45 | 2080 | Torino vs Lecce | 1.69 | 3.61 | 4.71 |
| 21:45 | 2127 | PAU FC vs St Etienne | 3.05 | 3.10 | 2.33 |
| 22:00 | 1500 | Valladolid vs Almeria | 2.29 | 3.23 | 3.08 |
| 22:00 | 1821 | Le Mans vs Red Star | 2.79 | 3.19 | 2.42 |
| 22:00 | 3362 | Real Oviedo vs Levante | 2.69 | 2.98 | 2.69 |
| 22:00 | 4691 | Middlesbrough vs Sunderland | 1.75 | 3.55 | 4.40 |
| 22:15 | 3686 | Breidablik vs Valur | 1.67 | 3.86 | 4.11 |
| 23:15 | 3594 | GD Chaves vs Rio Ave | 2.50 | 3.01 | 2.91 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# KMKM YATAMBA KUMALIZA NA MOTO ILIYOANZA NAO LIGI Z'BAR

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

MABINGWa watetezi wa Ligi Kuu Zanzibar, KMKM wamesema kasi waliyoanza nayo kwenye ligi hiyo msimu huu ndio mipango yao kwa msimu mzima.

KMKM katika mchezo wao wa kwanza Ligi Kuu Zanzibar juzi, iliibuka na ushindi wa mabao 4-0 dhidi ya timu ya Kundemba kwenye mchezo uliopigwa Uwanja wa Amaan majira ya saa moja usiku.

Bada ya matokeo hayo, Kocha Msaidizi wa timu hiyo, Ame Msimu, aliliambia Nipashe kuwa timu yao wamejiandaa kibingwa zaidi ili kuhakikisha mwanzo walio uanza unaendelea ili mipango yao ya mafanikio kwa msimu huu yatimie.

Alisema matokeo waliyoyapata ni ushindi mnono na mwanzo mzuri kwao kwenye ligi hiyo ambayo imeonyesha kuwa na ushindani mkali katika michezo hii ya awali.

Akizungumzia juu ya wapinzani wao hao, Msimu alisema walicheza mchezo mzuri katika kipindi cha pili ikilinganishwa na cha kwanza ambacho hadi mapumziko KMKM walikuwa mbele kwa mabao 3-0.

"Wapinzani wetu walitusumbua zaidi kipindi cha pili, nafikiri walijifunza makosa yao kupitia kipindi cha kwanza ambacho tulipata mwanya wa kupachika mabao matatu kabla ya kipindi cha pili kupata bao moja tu," alisema.

Kwa upande wa Kocha wa Timu ya Kundemba, Nadir Kijo, alisema makosa machache ndio yamesababisha kupoteza mchezo huo wa kwanza wa Ligi Kuu, hivyo wanajiandaa kwa mechi ya pili ambayo watashuka dimbani dhidi ya Wanajeshi wa Kipanga Septemba 13, mwaka huu.

Katika mchezo huo, mabao ya KMKM yalipachikwa nyavuni na Ilyasa Suleiman dakika ya 15 na 45, Yassin Mohmd dakika ya 25 na Is-haka Said dakika ya 90.

KMKM itashuka tena dimbani Septemba 13, mwaka huu dhidi ya Maafande wa Mafunzo.

Ligi Kuu Zanzibar mzunguko wa kwanza utatamatika leo, Jumatatu kwa kupigwa michezo miwili katika Dimba la Amaan majira ya saa 10 alasiri kwa Maafande wa KVZ kuwakaribisha Maafande wenzao wa Mafunzo, wakati majira ya saa moja usiku Timu ya Taifa Jang'ombe watawakaribisha Jamhuri kutokea Kisiwani Pemba.




Ofisa Mtendaji Mkuu wa Bodi ya Ligi nchini, Almasi Kasongo.

# *TPLB yapongeza klabu usajili Ligi Kuu*

**Na Adam Fungamwango**

BODI ya Ligi Kuu nchini (TPLB), imezipongeza klabu za Ligi Kuu kwa kufanya usajili kwa wakati, bila matatizo mengi kama ilivyokuwa miaka ya nyuma.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa Bodi hiyo, Almasi Kasongo, alisema mpaka dirisha lilipofungwa Agosti 31, mwaka huu hakukuwa na klabu za Ligi Kuu, Ligi ya Championship na Ligi Daraja la Pili, zilizoshindwa kukamilisha usajili, akisema ni maendeleo makubwa kwenye soka la Tanzania.

"Nizipongeze klabu kwa kukamilisha usajili kwa wakati, tofauti na miaka ya nyuma ambapo ilikuwa ikifika saa tano usiku kuelekea saa sita, asilimia 70 mpaka 80 zilikuwa zinakimbizana kumalizia usajili, wanajikuta wanakimbizana na kukamilisha matakwa ya mchezaji ili kukamilisha dili lake wakati mwingine mpaka kabla ya dakika tano dirisha kufungwa," alisema Kasongo.

Alisema sababu kubwa iliyosababisha klabu kuwa na uelewa ni Shirikishisho la Soka Nchini (TFF) na TPLB kabla ya usajili kukutana na mameneja na kuwapa semina ya jinsi gani ya kutuma majina na pia msimu huu kumekuwa na mfumo rafiki tofauti na ule wa awali.

"Tumepata mfumo rafiki zaidi tofauti na ule tuliokuwa nao na mameneja tumewapa mafunzo jinsi gani ya kufanya, na wao pia tunawapongeza kwa sababu wameongea na klabu zao kuona ni jinsi gani wanaweza kuifanya kazi hiyo mapema zaidi, ilifikia wakati huko nyuma muda mfupi kabla ya dirisha ndiyo kila klabu inatuma majina ya wachezaji wao mpaka mfumo unazidiwa kiasi cha kwamba hakuna anayeingia wala anayetoka," alisema.

Agosti 31, klabu zilikamilisha usajili wa Ligi Kuu Tanzania Bara msimu wa 2022/23, huku dirisha dogo likitarajiwa kufunguliwa Desemba, mwaka huu.

# Michezo

Jumatatu Septemba 5, 2022

Nipashe




Tuchel asifu uamuzi VAR, Moyes aponda UKURASA 21

SUBIRINI...



Dejan Georgijevic, akiwa mazoezini na wachezaji wenzake wa Simba. **PICHA: MAKTABA**

# Dejan: Simba tulieni nitafunga sana tu

## ●●● Ataja sababu kushindwa kutupia mabao huku akieleza sasa mambo yameanza...

**Na Saada Akida**

LICHA ya baadhi ya mashabiki wa Simba kuendelea kuwa na hofu kuhusu ubora wa mshambuliaji wao, Dejan Georgijevic, straika huyo raia wa Serbia amewataka kushusha presha kwa kuwa baada ya muda mfupi atakuwa amezoea mazingira na uchezaji wa kikosi hicho kabla ya kuanza kutikisa nyavu katika michezo iliyopo mbele yao.

**Simba ililazimika kumsajili Dejan baada ya kukosa saini ya Cesar Manzoki aliyekuwa bado ana mkataba na Vipers ya Uganda, ambaye hata hivyo amejiunga na Dalian Profesional Football Club ya China.**

Hata hivyo, tangu Dejan asajiliwe Simba, ameifungia bao moja kwenye mechi mbili za Ligi Kuu, alizocheza akitokea benchi kipindi cha pili, goli ambalo lilianza kupunguza hofu kuhusu uwezo wake wa kucheka na nyavu kwa mashabiki.

Lakini hofu hiyo kwa Dejan iliibuka tena hivi karibuni baada ya kucheza kwa dakika zote 90 bila bao waliposhuka dimbani nchini Sudan dhidi ya wenyeji wao, Al Hilal, kwenye mechi maalum ya kirafiki kujiandaa na michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

Kukata tamaa huko kwa baadhi ya mashabiki kuliendelea tena Jumamosi iliyopita baada ya Dejan kushindwa kuonyesha cheche zake huku akikosa bao la wazi katika mechi ya kirafiki ya kimataifa dhidi ya Arta Solar 7 ya Djibouti iliyopigwa Uwanja wa Uhuru, Dar es Salaam na Simba kulala kwa bao 1-0.

Lakini akizungumza na gazeti hili jana, Dejan alisema tayari ameanza kupata uelewano mzuri uwanjani na wachezaji wenzake, hivyo ana matarajio makubwa ya kufanya vizuri na kufunga sana katika mechi watakazocheza wakianza dhidi ya KMC FC keshokutwa, Jumatano katika Uwanja wa Benjamin Mkapa.

Alisema hajali kuhusu wimbo unaoimbwa "wa lete mzungu, lete mzungu..." na kuwa maarufu kwa mashabiki na wadau wa soka, zaidi ya yeye kuhakikisha anawapa furaha mashabiki kwa kutumia vema nafasi anazopata na kuwaletea ushindi.

"Najua mashabiki wanataka furaha na kufanya vizuri michezo iliyopo mbele yetu, tayari nimeanza kuzoea mazingira na mashabiki watarajie kupata mambo mazuri na kufunga katika kila mechi iliyopo mbele yetu," alisema Dejan.

Alisema atapambana na kujitoa kwa ajili ya kufanya kila linalowezekana kupata kilicho bora kwa ajili ya timu ikiwamo kufunga mabao na kuwapa furaha mashabiki wao.

Dejan alifunga bao la pili wakati Simba ikishinda 2-0 dhidi ya Kagera Sugar kwenye mechi ya Ligi Kuu iliyopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa Agosti 20, mwaka huu.

Simba ambayo ipo kileleni mwa msimamo wa Ligi Kuu ikiwa na pointi sita na mabao matano huku ikiwa haijaruhusu nyavu zake kutikishwa, inatarajia kuikaribisha KMC FC keshokutwa, Jumatano kwenye mechi ya ligi hiyo itakayopigwa Uwanja wa Mkapa saa moja usiku.

Baada ya mchezo huo, Simba itakwea 'pipa' kuelekea nchini Malawi tayari kwa mchezo wao wa kwanza wa hatua ya awali wa Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya wenyeji wao, Nyasa Bigi Bullets.

## Sababu kichapo Stars hiki hapa

**Adam Fungamwango na Hadija Mngwai**

WAKATI Kaimu Kocha Mkuu wa Timu ya Taifa ya Tanzania, Taifa Stars, Honour Janza, akisema kikosi chake kilitengeneza nafasi nyingi za kufunga, lakini hawakuweza kuzitumia kama wenzao, nyota wa zamani wa timu hiyo, Dua Said, amesema tatizo kubwa ni wachezaji wa sasa kutokujituma ipasavyo.

Taifa Stars imetolewa rasmi na Uganda katika mbio za kuwania kufuzu Fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika kwa Wachezaji wa Ndani (CHAN), zitakazofanyika mwaka nchini Algeria baada ya kutupwa nje kwa jumla ya mabao 4-0 kutokana na kipigo cha bao 1-0 nyumbani kabla ya Jumamosi kuchapwa 3-0 ugenini.

Akizungumza juzi baada ya kutolewa kwa kuchapwa mabao 3-0 kwenye Uwanja wa St Mary Chitende nchini Uganda dhidi ya The Cranes, kocha huyo alisema walikwenda nchini Uganda kusaka matokeo, lakini walitakiwa wawe imara dakika 25 za kipindi cha kwanza, ila baada ya kufungwa bao ikawa ni mzigo mkubwa kuweza kurudisha na kupata mabao ya ushindi.

Hata hivyo alisema vijana wake waliendelea kupambana na kupata nafasi nyingi kipindi cha pili, lakini hawakuweza kuzitumia huku wenzao wakifanikiwa kuzibadili kuwa mabao.

Hata hivyo wakati kocha huyo akisema hayo, Dua Said aliliambia Nipashe kuwa wachezaji wa sasa wamekuwa hawajitumi licha ya kulipwa vizuri na Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), wakiwa na Taifa Stars.

"Wachezaji wa sasa hawajitumi kama ilivyokuwa huko nyuma katika kipindi chetu, tulikuwa tukicheza kwa kujituma na mafanikio yalikuwa yakionekana licha ya kulipwa kidogo.

"Lakini wachezaji wa sasa wamekuwa hawajitumi ipasavyo licha ya kulipwa vizuri, wamekuwa hawana morali kama tulivyokuwa sisi," alisema Dua.


9 770856 541002 >

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042